# TUNAWEZA KUJUA MUNGU?

**PAR R.E. HARLOW**

**Mfasiri : G.I. Harlow**

**EVERYDAY PUBLICATIONS INC.**
**310 Killaly St. W.**
**Port Colborne ON L3K 6A6**
**Canada**

Copyright © 1973 Everyday Publications Inc.

# UTANGULIZO

Kitabu hiki kinafundisha ya kwamba TUNAWEZA kujua Mungu, na kinatujulisha mambo mengi juu ya Mungu. Mwandishi wa kitabu hiki alitaja mashairi mengi ndani ya Biblia kuhakikisha maneno aliyoandika. Vizuri usome mashairi haya yote ndani ya Biblia yako pamoja na kuomba Bwana kukufahamisha maana yao. Kama maneno mwandishi wa kitabu hiki aliyoandika yakipatana na maneno unayosoma ndani ya Biblia, amini maneno yenyewe. Kama Biblia ikikuagiza kufanya kitu fulani, tii maagizo haya. Ukijifunza kweli fulani, toa mashukuru kwa Bwana Mungu na fundisha kweli hii kwa watu wengine vilevile.

ISBN 0-919586-193-7

*Imprimé au Canada*

Copyright © 1973 Everyday Publications Inc.

## FAHIRISI


*Ukurasa*

MUNGU YUKO 5

TUNAWEZA KUJUA MUNGU? 6

BIBLIA INAFUNDISHA NINI JUU YAKE YENYEWE? 10

TUNAWEZA KUJUA NINI JUU YA MUNGU? 13

MUNGU - BABA, MWANA, NA ROHO MTAKATIFU 16

MUNGU BABA 18

KRISTO
- Kristo ni Mwana wa Mungu? 22
- Kazi ya Mwana wa Mungu mbele ya kuja Kwake duniani 24
- Mwana wa Mungu aligeuka Mtu 25
- Utu mkamilifu wa Mwana wa Mungu 27
- Kazi ya Mwana wa Mungu hapa duniani 28
- Mauti, ufufuko na kurudi Kwake mbinguni 29
- Kazi ya Kristo kwa wakati wa sasa 31
- Kurudi kwa Kristo mara ya pili 33

ROHO MTAKATIFU
- Roho Mtakatifu ni kama mtu 34
- Uungu wa Roho Mtakatifu 34
- Kazi ya Roho Mtakatifu 35

MALAIKA
- Kuumbwa kwa malaika 38
- Kuanguka kwa malaika kwa zambi 39
- Kazi ya malaika 40

MTU 44


Copyright © 1973 Everyday Publications Inc.

*Ukurasa*

WOKOVU
- Hitaji la wokovu 47
- Msingi wa wokovu 50
- Kawaida ya wokovu 54
- Wokovu unaleta nini kwa mtu? 57
- Matunda ya wokovu 61
- Baraka za wokovu 65

KANISA 69

MAMBO GANI YATATOKEA NYUMA? 73
- Kupelekwa kwa Wakristo mbinguni 74
- Mateso Makubwa 75
- Kuja kwa pili kwa Kristo 76

WAKATI WA KUJA
- Utawala wa miaka elfu moja 78
- Wakati wa milele 80

Copyright © 1973 Everyday Publications Inc.

# MUNGU YUKO

Watu wengi duniani hawaamini ya kwamba Mungu yuko. Wengine hawasemi wazi na kinywa chao Mungu hayuko, lakini mwenendo wao unaonyesha ya kwamba wanafikili hakuna Mungu. Wengine wanasema labda Mungu yuko lakini hakujifunua kwa watu. Basi tuwaze kwanza juu ya ulizo hili:

**Mungu yuko?**

Wakati tunapotazama dunia pahali tunapokaa, tunauliza, "Vitu hivi vilitoka wapi?" Miti na milima na viziwa na nyama na vitu vyote vingine vilifanyika namna gani? Kuna jibu moja tu kwa ulizo hili: Vilifanywa na Mungu. Mungu huyu ndiye Mungu Mwenye uwezo mkubwa. Biblia iliandikwa kwanza kwa Kiebrania. Maana ya neno lililotumiwa kwa Kiebrania kwa "Mungu" ni "Mwenye uwezo."

Wakati tunapotazama karibu karibu vitu ambavyo vinatuzunguka, tunaona kila kitu kilifanywa kwa kazi fulani kusaidia mambo yote duniani kuendelea vizuri. Basi nani alikuwa na akili ya kutosha kutengeneza maneno haya yote taratibu hivi? Mungu tu. Hakuna mtu!

Neno hili ni wazi kabisa. Hata hivi kuna watu wengine wanaosema hakuna Mungu. Basi tunauliza: Watu hawa wanaweza kujua namna gani ya kwamba hakuna Mungu? Mtu akisema hakuna Mungu, ni kama anasema yeye mwenyewe anajua maneno yote, na amefika pahali pote ulimwenguni. Kama sivyo, namna gani anaweza kujua hakika hakuna Mungu? Labda Mungu anakaa juu ya nyota moja mbali sana na dunia, au pahali pengine mtu wa dunia asipoweza kufika.

Si akili kusema hakuna Mungu. Kwa kuweza kusema hivi inakupasa kujua maneno yote na kuwa pahali pote kwa saa moja! Ni kusema wewe mwenyewe ni Mungu kwani mambo kama haya hayawezekani kwa watu. Kwa sababu hii Neno la Mungu linamwita mpumbavu mtu yule anayesema Mungu hayuko. "*Mpumbavu*

Copyright © 1973 Everyday Publications Inc.

*anasema moyoni mwake: Hakuna Mungu*" (Zaburi 14:1). Ni akili kupita kusema, "Sijui kama Mungu yuko au sivyo."

Mimi ninawaza ni heshima kubwa sana kwa sisi watu kuweza kujua Mwenyezi Mungu!

Watu wengine wanasema évolution inahakikisha ya kwamba Biblia si kweli. Evolution inafundisha ya kuwa zamani sana, kwa mwanzo kabisa, kulikuwa tu na kitu kidogo fulani. Kitu hiki kiiongezeka polepole, hata kiligeuka kuwa samaki, halafu miaka mingi nyuma samaki aligeuka nyama, na mwishoni mtu. Basi tunauliza: Kitu kidogo kile kilitoka wapi? Kilianza namna gani? Kilipata uzima namna gani? Ni Mungu tu anayeweza kupatisha uzima na kuchunga uzima wa kila kitu. Ni Yeye aliyeanza dunia hii na kuilinda.

Unavaa saa kwa mkono? Siku moja umeifungua na kutazama ndani? Ninazani ulishangaa wakati ulipoona vipande vidogo vidogo vingi ndani yake. Halafu rafiki yako akikuambia habari za mtu mmoja anayefanya saa kwa njia ya kuweka vipande hivi ndani ya bakuli na kuvitikisa, ungemwamini? Wapi! Unajua mtu mwenye akili nyingi tu anaweza kuunganisha vipande vidogo vyote vya saa pamoja kuwa saa nzima inayoweza kutembea vizuri. Vipande hivi haviwezi kamwe kukutana pamoja peke yao na kugeuka saa nzuri kwa njia ya kutikiswa ndani ya bakuli! Vivyo hivyo dunia hii ya ajabu haikufanyika peke yake bila Mungu.

# TUNAWEZA KUJUA MUNGU?

Kama Mungu yuko, tunaweza kuuliza maneno mane juu yake:

**1. Mungu ALIWEZA kujifunua Mwenyewe?**

Tumesema mbele ya kwamba maana ya "Mungu" ni "Mwenye Uwezo". Sisi watu tunaweza kusemezana pamoja. Ninaweza kukuambia mawazo yangu. Basi Mungu anaweza kufanya vivi hivi. Hakuumba viumbe wanaoweza kufanya mambo ambayo Yeye Mwenyewe hakuweza kuyafanya! Vilevile ingekuwa faida gani kwa Mungu kuumba watu kama asipoweza kujifunua kwao?

**2. ILIPASA Mungu kujifunua kwa watu?**

Mungu alifanya watu na zamiri ambayo inawajulisha ya kwamba mambo mengine ni mema na mengine ni mabaya. Anajua Yeye

Mwenyewe neno gani ni zuri na neno gani ni baya, na anataka watu kufanya yaliyo mema. Kama ni hivi, sharti awapashe waziwazi mambo gani ni mambo mazuri au maovu. Hawezi kuwaazibu kwa kutenda maovu kama asipowafundisha mbele mambo gani ndiyo maovu.

**3. Mungu ALITAKA kujifunua kwa watu?**

Tuliona mbele ya kwamba Mungu ALIWEZA kujifunua kama akitaka. Basi kwa sababu gani atataka? Kwanza ili watu waweze kujua mambo gani ni mema, na vilevile hata waweze kumjua na kumpenda Yeye. Aliumba watu ili aweze kuwaonyeshea mapendo yake na haki yake.

**4. Mungu ALIJIFUNUA kwa watu KWELI?**

Kama alijifunua kwao, alijifunua *namna gani* na *pahali gani?* Mungu ni namna gani? Anataka mimi nifanye nini? Maulizo haya ni maulizo makubwa.

Ndiyo, Mungu alijifunua kwa watu. Alijifunua kwao katika Biblia. Ndani ya Biblia tunasoma ya kwamba kitabu hiki ni Neno la Mungu. Tunasoma ndani ya vitabu vingine kusema vitabu hivi ni Neno la Mungu vilevile, lakini hakuna neno ndani yao linalohakikisha ya kwamba ni kweli.

Namna gani tunaweza kujua ya kuwa Biblia, Biblia peke yake, ni habari toka Mungu? Tutataja mambo manane yanayohakikisha neno hili.

1) *Umoja wa Biblia*. Kabisa kabisa Biblia ni vitabu 66 vinavyofungwa pamoja kuwa kitabu kikubwa kimoja. Vitabu hivi viliandikwa na watu karibu 40. Wengine walikuwa wafalme, wengine wachungaji kondoo, wahubiri, walimaji shamba, makuhani. Waliandika kwa nyakati mbalimbali. Mwandishi wa mwisho aliandika kitabu chake karibu miaka 1500 nyuma ya mwandishi wa kwanza. Hata hivi vitabu hivi 66 vilivyoandikwa kwa nyakati mbalimbali na watu mbalimbali vinapasha vyote juu ya Mtu mkubwa mmoja, ndiye Bwana Yesu Kristo. Ndani ya Agano la Kale tunasoma ya kwamba ATAKUJA na atakuwa Mwokozi. Katika Agano Jipya tunasoma ya kwamba AMEKUJA kweli na amekufa msalabani ili aweze kuwa Mwokozi wetu. Hivi tunaona umoja wa kushangaza ndani ya Biblia.

2) *Mambo yaliyotokea mia za miaka mbele* yanaonyesha ya kuwa Biblia ni kweli Neno la Mungu. Watu wenye kutafuta maneno yaliyotokea zamani wanachimba udongo juu ya miji ya zamani.

Nyuma ya kuondosha udongo wote juu ya miji hii wanaweza kupata ndani ya mavunjiko yao vitu vingine vinavyoweza kuwasaidia kufahamu historia ya zamani. Tena na tena wamepata maandiko ndani ya miji hii yanayoonyesha kwamba Biblia ni kweli.

Huhitaji kufahamu kila neno linaloandikwa ndani ya Biblia mbele ya kuweza kuiamini. Maneno mengine ni magumu sana na tunashindwa kuyafahamu, lakini hata hivi tunaweza kuyaamini pamoja na maneno yote mengine ambayo Biblia inatupasha.

Watu wengine wanasema Biblia si kweli kwa sababu hawaamini mishangao na maajabu yanayoandikwa ndani yake. Wanasema mambo kama haya hayawezekani. Lakini fikili kwanza. Kama kuna Mungu, kwa sababu gani hataweza kufanya mambo yanayoshinda watu? Mungu ni Mwenye uwezo wote. Sharti kitabu kinachopasha habari za Mungu kipashe habari za kazi zake za ajabu. Maajabu hayaonyeshi kwamba Biblia si kweli, lakini yanahakikisha ya kuwa inatupasha kweli juu ya Mungu.

3) Neno lingine linaloonyesha ya kwamba Mungu amejifunua ndani ya Biblia ni *kutimia kwa unabii*. Miaka mingi mbele ya kuzaliwa kwa Bwana Yesu Kristo watumishi wa Mungu waliandika ndani ya Biblia ya kwamba Kristo atakuja. Walipasha wakati gani na pahali wapi na namna gani atazaliwa. Walipasha habari nyingine vilevile zilizotokea miaka mingi nyuma. Ndani ya Agano Jipya tunasoma ya kwamba maneno haya yalitokea kweli. Basi namna gani watu hawa waliweza kujua maneno yatakayotokea miaka mingi nyuma? Mungu tu aliweza kuwajulisha.

4) *Biblia inatufahamisha ya kwamba sisi ni wenye zambi.* Ndani ya Agano la Kale tunasoma sheria takatifu ya Mungu. Sheria hii ilikuwa takatifu kabisa hata hakuna mtu aliyeweza kuitii kabisa kabisa kwa kila neno. Katika Agano Jipya tunapata habari za maisha ya Mtu mkamilifu mmoja, Bwana Yesu Kristo. Yeye peke yake alitimiza sheria ya Mungu. Watu elfu elfu wakisoma Biblia wanafahamu ya kwamba wao si watu wazuri kwa macho ya Mungu. Wanasoma habari za namna ya mwenendo Mungu anaotaka kwao na wanapata haya.

5) Kama Biblia ingalitupasha neno hili tu kama tusipoweza kuwa na salama na furaha kamwe. Lakini asante kwa Mungu kwani Biblia ina habari nyingine kwa sisi vilevile. Inatupasha habari za Mwokozi. Hizi ndizo habari za ajabu kupita habari zote pia zilizoandikwa ndani ya vitabu vyote vingine.

Kila dini inafundisha watu nini inawapasa KUFANYA. Biblia

peke yake inatupasha ya kwamba kila neno lililohitajiwa kwa wokovu wetu LIMEFANYWA. Bwana Yesu Kristo alibeba azabu ya Mungu kwa zambi zetu.

Hakuna mtu aliyeweza kufikili njia nzuri namna hii kuokoa watu. Iliweza kutoka kwa nia ya Mungu tu. Neno hili linaonyesha vilevile ya kuwa Biblia imetoka kwa Mungu.

6) *Habari hizi za Kristo na kazi yake tunazopata ndani ya Biblia zina uwezo kabisa.* Maisha na mwenendo wa milioni za watu imegeuzwa kabisa kwa njia ya Habari Njema ya Kristo. Watajiri na watu masikini, wenye kupenda dini na wale waliosema hawaamini ya kwamba Mungu yuko — wengi wao wamepata salama rohoni ndani ya Kristo.

7) Watu wengine hawaamini Biblia kwa sababu ni kitabu cha zamani kabisa. Wanataka kitu kipya, kitabu kilichoandikwa kwa wakati wa sasa. Lakini hata uzee wa Biblia unaonyesha ya kwamba ni kitabu cha namna nyingine kabisa. *Mungu aliichunga miaka hii yote kufika leo.* Ndiyo, kuna vitabu vingine vilevile vilivyo vizee sana. Lakini hata kama watu walijaribu tena na tena kuharibu Biblia, Mungu ameichunga kufika leo — ni Neno lake kwa sisi.

8) Basi kama Biblia ni kitabu cha zamani sana kisicho na faida kwa sisi leo, na kama kweli watu wamepata makosa mengi ndani yake, utafikili watu hawatataka kuinunua tena. Sivyo? Ndivyo, tungefikili hivi. Lakini kabisa kabisa kila mwaka hesabu ya Biblia watu ambazo wanazinunua inapita hesabu ya mwaka uliopita. Biblia nzima au sehemu yake imetafsiriwa ndani ya lugha zaidi ya 1200. Kila mwaka milioni za Biblia au sehemu za Biblia zinachapwa na kuuzwa. Neno hili linahakikisha kwamba ni kitabu cha faida nyingi kwa watu wa sasa, na ya kuwa makosa si ndani yake kwa sababu ni Mungu ambaye aliiandikisha.

Ndiyo, Biblia ni kitabu cha ajabu kabisa, kupita vitabu vyote vingine duniani. Ni namna nyingine kabisa na vitabu vyote vingine. Watu wasingaliweza kufikili kuandika maneno yanayoandikwa ndani yake. Kweli ni Neno ia Mungu. Kweli Mungu alijifunua kwetu ndani ya Biblia.

*KWELI NI NINI?*

*Ni maneno Mungu anayosema juu ya jambo fulani.*

# BIBLIA INAFUNDISHA NINI JUU YAKE YENYEWE?

Tumeona ya kama Mungu amejifunua ndani ya Biblia. Habari nyingine ndani ya Biblia Mungu alifunua Yeye Mwenyewe kwa mwandishi, kama habari za kuumbwa kwa dunia. Adamu asingaliweza kujua namna gani dunia hii iliumbwa kama Mungu asingalimwambia. Sehemu nyingine za Biblia zinatupasha nini mwandishi aliyoona au kujifunza karibu na watu wengine. Waandishi hawa waliongozwa na Mungu kuandika mengine ya mambo yaliyotokea na kuacha mengine. Kwa sababu gani iliwapasa kuandika mambo fulani tu? Roho Mtakatifu ametupa sisi ndani ya Biblia habari zote na mafundisho yote tunayohitaji, lakini si mambo mengine kupita yale. *"Kila andiko limepewa na Mungu, na linafaa kwa mafunisho, na kwa kuonya watu juu ya makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa mafundisho katika haki; ili mtu wa Mungu awe mkamilifu, ametengenezwa kabisa kwa kila tendo jema"* (2 Timoteo 3:16-17).

## BIBLIA INASEMA YA KWAMBA MUNGU ALIWAONGOZA WALE AMBAO WALIIANDIKA

**Agano la Kale**

Ndani ya Agano la Kale tunasoma mara nyingi, *"Bwana amesema hivi"* au *"Mungu alisema na . . ."*. Tunakuta masemo kama haya mara elfu na zaidi ndani ya Agano la Kale. Kwa mfano, MUSA alisema ya kwamba Mungu alisema naye:

> "Mungu akamwita toka kati ya kijiti, akasema: Musa, Musa" (Kutoka 3:4).
>
> "Bwana akaniambia" (Torati 1:42).
>
> "Bwana akaniamuru" (Torati 4:14).

MANABII WOTE kumi na sita tunaopata unabii wao ndani ya Biblia, kuanza na Isaya kufika hata Malaki, walisema Mungu alisema nao.

BWANA YESU KRISTO vilevile alifundisha ya kwamba Agano la Kale ni Neno la Mungu. Ni kusema Roho Mtakatifu aliongoza watu kuandika maneno aliyotaka wayaandike. Alisema hivi juu ya

Sheria: Matayo 5:18; Marko 7:8

Manabii: : Yoane 6:45

Maandiko yote ndani ya Agano la Kale: Luka 16:29-31; Yoane 17:17.

MITUME waliamini ya kama Mungu aliongoza kuandika kwa Agano la Kale.

*Petro:*"alilosema Roho Mtakatifu zamani kwa kinywa cha Daudi" (Matendo 1:16).

"Watu walisema yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:21).

*Paulo:* "Roho Mtakatifu alisema vizuri na baba zenu, kwa kinywa cha nabii Isaya" (Matendo 28:25).

"Kila andiko limepewa na Mungu" (2 Timoteo 3:16).

**Agano Jipya**

Wakati Kristo alipokuwa hapa duniani, aliahidi wanafunzi wake ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja. Alisema, *"Roho Mtakatifu . . . atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote ambayo niliwaambia ninyi"* (Yoane 14:26). Neno hili liliwawezesha kuandika vitabu vya Habari Njema.

Bwana Yesu alisema vilevile, *"Wakati anapokuja yule Roho ya kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli"* (Yoane 16:13). Neno hili liliwawezesha kuandika barua za Agano Jipya ndani yao tunapata kweli zote za Mungu.

Kristo alisema vilevile ya kwamba Roho Mtakatifu atawaonyeshea maneno yatakayotokea nyuma (Yoane 16:13). Ahadi hii ilitimizwa; Yoane aliandika kitabu cha Ufunuo na watu wengine waliandika juu ya mambo yatakayotokea nyuma vilevile. Hivi tunaona ya kwamba Bwana Yesu alitayarisha wanafunzi wake kwa kazi ya kuandika Agano Jipya. Kazi hii iliongozwa na Mungu kama vile kuandika kwa Agano la Kale.

Waandishi wa Agano Jipya walifahamu ya kuwa Roho Mtakatifu aliwaongoza ndani ya maneno waliyoandika.

*Paulo* alisema:

"Mungu aliyafunua kwetu kwa Roho yake" (1 Wakorinto 2:10).

"Maneno ambayo ninawaandikia ninyi . . . ni agizo la Bwana" (1 Wakorinto 14:37).

"Kwa ufunuo nilijulishwa siri hii . . . katika Roho" (Waefeso 3:3,5).

"Roho anasema waziwazi" (1 Timoteo 4:1).

Soma vilevile maneno Yoane aliyosema katika Ufunuo 1:1; 14:13; 19:9.

Petro na Paulo wao wawili walijua ya kuwa Habari Njema ilitoka kwa Mungu. Ona 1 Petro 1:12 na Wagalatia 1:12.

Watu hawa wote waliamini kabisa ya kama Mungu aliongoza kuandika kwa Agano la Kale. Roho Mtakatifu aliwaonyeshea ya kwamba kuandika kwa Agano Jipya kuliongozwa na Mungu vivyo hivyo. Katika 1 Wakorinto 15:3-4 vitabu vine vya Habari Njema vilihesabiwa kuwa sehemu ya Maandiko Matakatifu. Ndani ya mashairi haya tunasoma juu ya mauti, kuzikwa, na ufufuko wa Kristo sawasawa na Maandiko. Habari hizi ziliandikwa ndani ya vitabu vya Habari Njema. Katika 1 Timoteo 5:18 Paulo alitaja mashairi toka Torati na Luka na aliita vitabu hivi viwili "maandiko", ndiyo Maandiko Matakatifu. Katika 1 Petro 1:24-25 Petro aliita Habari Njema "Neno la Bwana" kama katika Isaya. Ndani ya 2 Petro 3:2 alitaja mitume na manabii pamoja, na ndani ya 2 Petro 3:16 alisema juu ya barua za Paulo pamoja na maandiko mengine sawasawa ni yote Neno la Mungu.

Hivi tunaona ya kwamba kuandika kwa sehemu zote za Biblia kuliongozwa na Mungu. Aliongoza kila neno. Paulo aliandika, *"si katika maneno yanayofundishwa na akili ya watu, lakini yanayofundishwa na Roho Mtakatifu"* (1 Wakorinto 2:13).

**Waandishi wa Biblia**: Lakini hata kama Mungu aliongoza kila neno lililoandikwa, unaweza kuona kwa njia ya maandiko yao kama waandishi wa Biblia walikuwa watu wa namna gani. Kwa mfano maandiko ya Yeremia ni namna nyingine kabisa na maandiko ya Isaya na Ezekieli.

**Maandiko ya kwanza**: Vitabu hivi vilipotea zamani. Bila shaka Mungu alitaka iwe hivi ili watu wasiviabudu kama vitu vitakatifu sana. (Ona 2 Wafalme 18:4.) Lakini tuna miigo mizuri sana ya maandiko haya ya kwanza. Miigo hii ni sawasawa na maandiko ya kwanza katika karibu mambo yote.

**Tafsiri**: Haiwezekani kwa tafsiri ya Biblia kuwa kamilifu kabisa katika kila neno. Lakini tafsiri tulizo nazo zinatosha kabisa kwa kutuongoza hapa duniani na kwa dunia itakayokuwa nyuma.

Mara nyingine waandishi wa Agano Jipya walitaka kuongeza mambo mengine ndani ya maandiko yao, lakini Roho Mtakatifu aliwazuiza. Waliongozwa kuandika mambo fulani tu, na kukatazwa kuandika mengine. Kwa mfano:

Katika kitabu cha Ufunuo Yoane alitaka kuandika maneno ngu-

rumo saba ziliyosema, lakini alikatazwa (Ufunuo 10:4). Mwandishi wa barua kwa Waebrania alitaka kuandika juu ya Melkisedeki (Waebrania 5:11), lakini alizuizwa. Yuda alitaka kuandika juu ya wokovu, lakini aliongozwa kuonya na kusukuma watakatifu kusimamia imani (Yuda 3).

Hivi Roho Mtakatifu aliongoza waandishi hawa wote wa Biblia kuandika mambo mengine na kuacha mengine. Basi sasa tuendelee kujifunza nini Mungu anasema nasi ndani ya Biblia.

# TUNAWEZA KUJUA NINI JUU YA MUNGU?

Ni neno zuri kabisa kuweza kujua Mungu! Tumeona ya kwamba Mungu amejifunua ndani ya Biblia. Basi Biblia inatuonyesha nini juu ya Mungu?

Biblia inatuambia maneno mengi juu yake. Tutataja sasa maneno kumi na mawili.

1. **Mungu ni roho** (Yoane 4:24). Yeye si mtu. Hana mwili wa namna yo yote. Ndani ya mashairi mengine katika Biblia tunasoma juu ya mkono wa Mungu, jicho la Mungu, vivi hivi. Maneno haya ni mfano tu kuonyesha ya kwamba Mungu ni Mwenye uwezo wote na anaweza kufanya mambo yo yote anayotaka, na anaweza kujua kila neno. Lakini tangu Mwana wa Mungu alipogeuka mtu, tunaweza kusema ya kwamba Mungu Mwana ana mwili.

2. **Hatuwezi kuona Mungu na macho** (1 Timoteo 1:17), kwani Yeye ni Roho. Watu hawawezi kuona roho. Hata kama hakuna mtu aliyeona Mungu katika utukufu wake wakati wo wote, Yesu Kristo, Mwana wake alimfunua kwa watu (Yoane 1:18). Yesu alisema, *"Ambaye aliniona mimi, ameona Baba"* (Yoane 14:9). Hata kama watu hawawezi kuona Mungu na macho yao wenyewe, wanaweza kujuana naye kwa njia nyingine. Kwa sababu haonekani kwa macho ya watu, amewakataza kufanya sanamu ya Mungu.

3. **Mungu ni wa milele** (Torati 33:27; Waroma 16:26). Hakuwa na mwanzo na hatakuwa na mwisho kamwe. Amekuwa tangu zamani na atakuwa kwa milele. Wakati vitu vyote vingine

visipokuwa bado, Mungu alikuwa. Mambo haya yanatushinda kufahamu, lakini hata hivi tunajua ni hivi. Mungu aliumba vitu vyote, lakini hakuumbwa Yeye Mwenyewe. Yeye asiyekuwa na mwanzo alianza vitu vyote.

4. **Mungu ni juu ya vitu vyote** (Zaburi 95:3). Aliumba viumbe vingi. Wengine ni wenye uwezo kabisa. Wengine waliasi Mungu. Lakini Mungu hakuumba viumbe watakaoweza kuwa na uwezo mkubwa kupita Yeye Mwenyewe. Vilevile hesabu ya viumbe hivi vyote pamoja haitoshi kwa kuweza kuzuiza Mungu asitimize makusudi yake. Mungu atakuwa siku zote juu ya vitu vyote na mwishoni atatimiza mambo yote aliyokusudi kuyafanya.

5. **Mungu ni Mwenye uwezo wote** (Yobu 42:2). *"Maneno yote yanawezekana kwa Mungu"* (Marko 10:27). Mungu aliyefanya vitu vyote anaweza kufanya neno lo lote analotaka na vitu na viumbe alivyoumba. Na bila shaka Mungu anaweza kufanya maneno viumbe ambavyo aliviumba wasiyoweza kufanya. Wakati Mungu anapofanya neno linaloshinda watu, anafanya ajabu au mshangao.

6. **Mungu anajua mambo yote** (Zaburi 139:1-4). Anajua kila neno, hata mawazo ya watu. Hatuwezi kumfichia hata moja.

7. **Mungu ni pahali pote** (Yeremia 23:24). Anaweza kujua na kuona mambo yote yanayofanyikana hapa duniani wakati wo wote. Hata hivi anakaa mbinguni (Torati 26:15). Lakini hata kama Mungu akiona kila neno, hapendezwi na maneno yote anayoona. Yeye ni mtakatifu na anachukia zambi.

8. **Mungu amejifunua** (Matendo 7:2). Watu hawawezi kuvumbua Mungu kwa nguvu yao wenyewe (Yobu 11:7), lakini kwa neema Mungu amejifunua kwao.

9. **Mungu ni sawasawa siku zote** (l Samweli 15:29; Malaki 3:6; Waebrania 6:18). Hawezi kutenda namna nyingine na namna alivyo. Hawezi kusema uwongo au kugeuka.

Mara nyingine tunasoma ndani ya Biblia ya kama Mungu amejuta (Yeremia 18:8). Maana yake si kusema Yeye Mwenyewe amegeuka namna nyingine, lakini mawazo yake juu ya watu yamegeuka kwa sababu ya matendo yao.

10. **Mungu ni Mwenye haki** (Zaburi 7:11; 11:7; Ufunuo 16:7). Hawezi kuacha zambi kupita bule. Sharti aihukumu, si neno kama ni nani aliyefanya zambi yenyewe.

11. **Mungu anatawala ulimwengu.** (Ulimwengu ni dunia yetu na nyota na mwezi na jua na dunia zote nyingine pamoja.) Sharti

ahukumu kwa haki. Amefanya hivi tangu zamani na atafanya hivi milele. *"Mwamuzi wa dunia nzima hatatenda kwa haki?"* (Mwanzo 18:25).

12. **Mungu ni mtakatifu** (Isaya 6:3). Anachukia zambi na hawezi kukubali zambi karibu naye. *"Wewe uliye na macho safi zaidi hata usiweze kutazama mabaya"* (Habakuki 1:13). Maana ya shairi hili si kusema Mungu *hawezi* kuona matendo maovu ya watu. Ni kusema hawezi kutazama matendo maovu bila kukasirika sana.

13. Mwishoni, na neno hili ni neno la kutushangaza zaidi, **Mungu ni mwenye neema**. Soma Kutoka 33:19 na 1 Yoane 4:8. Hatustahili hata kidogo kupokea neema ya Mungu — tunastahili hukumu tu. *"Mungu wa neema yote . . ."* (1 Petro 5:10). Neema ni machanganyiko ya wema, uzuri, rehema na mapendo ya Mungu.

Mungu ashukuriwe kwa neema na mapendo yake kwetu. Anatujua na maneno yetu yote, na kwa sababu Yeye ni Mwenye haki, ingempasa kutufukuza toka Kwake. Lakini kwa sababu Yeye ni Mwenye neema vilevile na anatupenda, ametengeneza njia kumwezesha kusamehe zambi zetu na kutufanyiza wana Wake. Kweli Mungu wetu ni Mungu wa ajabu. Ni furaha kubwa kujua ya kuwa baraka zake zote ni kwa sisi.

# MUNGU – BABA, MWANA, NA ROHO MTAKATIFU

1. Kuna Mungu mmoja tu.
2. Kristo ni mbalimbali na Mungu Baba, lakini ni Mungu vilevile.
3. Roho Mtakatifu ni mbalimbali na Mungu Baba, lakini Yeye vilevile ni Mungu.

Kwa mfano: *"Neno alikuwa pamoja na Mungu"*; *"Neno alikuwa Mungu"* (Yoane 1:1). Shairi hili linatufundisha ya kwamba Neno halikuwa sawasawa na Mungu, hata kama kwa mwanzo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Lakini shairi hili linasema vilevile, *"Neno alikuwa Mungu."* Shairi 14 la sura hii linaeleza ya kwamba Neno hili ni Kristo. Basi namna gani Kristo, Neno la Mungu, anaweza kuwa Mungu, bila kuwa sawasawa na Mungu?

Katika Yoane 10:28 Yesu alisema juu ya mkono wake mwenyewe na katika shairi 29 juu ya mkono wa Baba yake. Ni Baba ambaye alimpa Kristo kondoo. Hata hivi katika shairi 30 anasema, "Mimi na Baba yangu tu mmoja."

Katika sura 1 ya Waebrania mwandishi anataja shairi moja toka Zaburi 45. Ndani ya Waebrania 1:8 Mwana anaitwa Mungu: *"Kiti chako cha ufalme, Mungu, ni cha milele na milele."* Lakini katika shairi 9 Mungu anatia Mwana mafuta ya furaha. Basi namna gani Mwana anaweza kuwa Mungu na hata hivi kuwa namna nyingine na Mungu?

Mashairi mengine ndani ya Biblia yanayosema juu ya Roho Mtakatifu yanafanana na mashairi haya. Nyuma kidogo tutaona ya kama Roho Mtakatifu ni Mungu. Lakini Baba na Mwana walituma Roho Mtakatifu duniani. Hivi, hata kama kuna Mungu mmoja tu, Yeye ni tatu ndani ya moja, Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Tutaweza kueleza mambo haya namna gani? Hatuwezi kuyafahamu wala kuyaeleza, lakini hata hivi tunajua ni kweli!

Kuna mambo mengine ambayo yanatushinda kufahamu vivyo hivyo. Tunatumia umeme kupata nuru nyumbani mwetu, kutembe-

za machines namna namna na kufanya kazi mbalimbali, lakini hatujafahamu bado mambo yote juu ya umeme hata kidogo. Tunatumia nuru bila kufahamu siri zake zote. Tunajua vitu vingine ni hai, na vingine vinakosa uzima, lakini tunashindwa kuvipatisha uzima. Basi kama tukishindwa kufahamu vitu ambavyo Mungu aliviumba, tusishangae kama tusipoweza kufahamu maneno yote juu ya Mungu Yeye Mwenyewe!

Kujua na kuamini maneno ambayo Biblia inatufundisha juu ya Mungu ni vizuri kuliko kujaribu kueleza kila neno. Siku nyingine wakati tutakapofika kwake tutafahamu vizuri kupita. Kwa sasa tumwabudu na kumtukuza kwa ukubwa wake na uzuri wake wote.

# MUNGU BABA

Mungu anaitwa “Baba” ndani ya Biblia kwa njia mbalimbali tano.

**Anaitwa Baba ya Kristo.**

Bwana Yesu alisema NA Baba yake au JUU YA Baba yake mara nyingi: mara 20 katika Matayo; mara mbili katika Marko; mara 11 katika Luka; mara 62 katika Yoane; na mara tatu katika Ufunuo. Paulo alisema mara sita juu ya Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo. Petro alisema vivyo hivyo ndani ya barua yake ya kwanza, na Yoane alitumia maneno yanayofanana na haya mara mane.

Mungu aliita Kristo Mwana wake. Alisema mara mbili toka mbingu: “Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ninapendezwa naye” (Matayo 3:17; 17:5).

Lakini tusifikili Mungu alikuwa na mke au aliumba Mwana wake! Ndani ya sura inayofuata sura hii tutaona mashairi yanayoonyesha wazi kabisa ya kwamba Mwana ni tangu milele na hakuumbwa. Hakuwa na mwanzo. Lakini tuwaze hapa juu ya maneno mawili yaliyosemwa juu ya Bwana Yesu:

1) *Mwana pekee* (Yoane 1:14). Yoane aliita Bwana Yesu hivi mara tano ndani ya Habari Njema yake na ndani ya barua yake ya kwanza.

2) *Mzaliwa wa kwanza* (Wakolosayi 1:18). Maneno haya yalitumiwa juu ya Kristo mara saba. Ndiyo, Bwana Yesu alikuwa kweli mzaliwa wa kwanza wa Maria, mtoto wake wa kwanza, lakini mara zote nyingine wakati maneno haya yalipotumiwa juu ya Kristo, yanaonyesha ya kwamba Yeye anapita watu kwa njia ya ukubwa na heshima, si kwa njia ya kuzaliwa mbele yao. Katika Wakolosayi 1:15 anaitwa mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote, katika Wakolosayi 1:18 mzaliwa wa kwanza kutoka katika wafu, na kwa Waroma 8:29 mzaliwa wa kwanza katikati ya ndugu wengi.

Kwa wakati wa Agano la Kale ilikuwa desturi ya watu kumpa mwana mzaliwa wa kwanza baraka kubwa kuliko wana wengine. Lakini mara nyingine mwana mwingine alipewa baraka hii, si yule aliyezaliwa kwanza katika jamaa hii. Kwa mfano Semu, Isaka, Yakobo, Yuda, na Solomono walipewa baraka ya mzaliwa wa kwanza hata kama hawakuzaliwa kwanza.

Kristo aliitwa “Mzaliwa wa kwanza” kuonyesha Yeye ni mwe-

nye heshima zaidi, si ya kwamba alizaliwa kwanza, kwani hakuzaliwa – alikuwa tangu mwanzo.

**Anaitwa Baba ya watu**

(1) Kama Mwumba, Mungu anaitwa Baba ya watu wote. Soma Luka 3:38; Matendo 17:29. Lakini watu walianguka kwa zambi na hivi hawana ruhusa sasa kumwita Baba yao. Mungu anasema nao, *"Kama mimi ni baba, heshima yangu ni wapi?"* (Malaki 1:6).

(2) Waisraeli waliitwa watoto wa Mungu mara nyingi (Kutoka 4:22; Torati 14:1; Isaya 1:2). Mungu aliitwa Baba yao vilevile (1 Mambo 29:10; Isaya 63:16; Yeremia 3:19). Lakini ndani ya mashairi haya tunasoma juu ya taifa la Israeli, si juu ya Waisraeli mmoja mmoja.

(3) Ndani ya mashairi machache katika Agano la Kale Mungu anaitwa Baba ya watu wengine. Anaitwa Baba ya yatima katika Zaburi 68:5. Katika 1 Mambo 28:6 alijiita Mwenyewe Baba ya Solomono.

(4) Lakini zaidi Mungu anaitwa Baba ya waamini wa wakati wa sasa. Neno hili ni neno kubwa na tunataka kuuliza:

## MTU ANAWEZA KUINGIA NDANI YA JAMAA YA MUNGU NAMNA GANI?

Kuna njia tatu kuingia ndani ya jamaa fulani hapa duniani. Njia hizi zote ni mfano wa mwamini.

Kwa njia ya **kuzaliwa**. Kila mtoto anazaliwa ndani ya jamaa ya baba na mama. Vivyo hivyo mtu anapokea uwezo kuwa mtoto wa Mungu na kuzaliwa ndani ya jamaa yake wakati anapoamini jina la Bwana Yesu Kristo na kumpokea kuwa Mwokozi wake (Yoane 1:12-13).

Kwa njia ya **kupokewa kama mwana**. Unaweza kupokea mtoto wa watu wengine ndani ya jamaa yako kuwa mtoto wako mwenyewe. Neno hili linakubaliwa na sheria ya inchi. Kwa mfano binti ya Farao alipokea Musa na kumpatisha nguvu kama mtoto wake mwenyewe.

Kwa njia ya ndoa mtu anaweza kugeuka mke wa mwana wa nyumba au bwana ya binti ya nyumba. Mama ya bwana ya Ruta aliita Ruta "binti yangu" (Ruta 3:1). Baba ya mke wa Daudi aliita Daudi "mwana wangu" (1 Samweli 24:16). Katika Agano Jipya Kanisa ni Bibi Arusi ya Kristo (Waefeso 5:25). Sisi Wakristo tuko ndani ya jamaa ya Mungu (Waefeso 3:15).

## KWA SABABU GANI NI NENO ZURI SANA KUWA NDANI YA JAMAA YA MUNGU?

Wale wanaozaliwa tena na kuingia jamaa ya Mungu wana-barikiwa kwa njia nyingi.

Hapa duniani yatima anahuzunika kwa sababu hana baba. Ndani ya dunia hii kubwa, ni furaha kabisa kujua ya kama Mungu ni Baba yangu (Yoane 20:17)!

Kila mwana wa Mungu ana pahali anapoweza kuita "kwetu". Ana ruhusa kuingia nyumbani mwa Mungu mbinguni. Hapa duni-ani tuko wasafiri, lakini safari yetu inatupeleka kwa ikao letu mbi-nguni. Kristo ametutangulia kulitayarisha (Yoane 14:2).

Mungu ni mapendo. Kama Mungu ni Baba yangu, ninaweza kujua kabisa ya kwamba ananipenda (Yoane 16:27). Bila shaka atanichunga na kunipatia kila kitu ninachohitaji (Matayo 6:32-33).

Kwa sababu ninajua mapendo na uwezo wa Baba yangu, sihitaji kusumbuka juu ya mambo yaliyo mbele yangu, mambo yataka-yotokea nyuma. Yesu alisema, *"hakuna mtu anayeweza kuwa-nyanganya toka mkono wa Baba yangu"* (Yoane 10:29). Ninaweza kujua kabisa ya kwamba sitapotea kamwe!

Mungu Baba anafahamisha kila mwana ya kuwa ana uzima wa milele hata sasa hapa duniani. Anaahidi vilevile kumpa uriti kwa wakati wa kuja. Mtu asiye na uzima hawezi kupokea uriti. Wana tu ni wariti (Waroma 8:17).

Kuna baraka kubwa nyingi nyingine kwa wale walio ndani ya jamaa ya Mungu.

## NINI INATOKEA KAMA MTOTO WA MUNGU AKIFANYA ZAMBI?

Labda ingekuwa vizuri kuliko kuuliza, "Nini inatokea WAKATI mtoto wa Mungu anapofanya zambi?" Hakuna mtu aliye mtoto wa Mungu kweli anayetaka kufanya zambi. Lakini hakuna mmoja katikati yetu anayeweza kusema, "Sina zambi."

Kama mtoto wa Mungu akikosea Baba yake, Mungu atamfukuza toka jamaa yake? Sivyo, lakini atamwazibu kwa sababu Yeye ni mtoto wake. Mungu anapenda watoto wake. Hawezi kuwafukuza toka jamaa yake kwa sababu ya zambi zao, lakini hawezi kuwaacha kuendelea kwa zambi na salama. Soma Waebrania 12:5-11. Kila mtu aliye mtoto wa Mungu kweli anaazibiwa ili aweze kushiriki utakatifu na salama ya Mungu Baba.

Kama mtoto wa Mungu asipotubu wakati Mungu anapomwazibu, kama asipokuwa na huzuni kwa sababu ya zambi zake na kujaribu kuziacha, labda Baba atampeleka kwake mbinguni. Neno hili ni vizuri kuliko kumwacha hapa duniani kuleta haya juu ya jina la Baba. Wakristo wengi wa Korinto walikufa kwa sababu ya matendo yao mabaya (1 Wakorinto 11:30). Yoane alisema inatupasa kuombea ndugu aliyeanguka ndani ya zambi au anayeendelea kwa zambi, isipokuwa ni zambi iliyo ya mauti (1 Yoane 5:16).

Wakati tutakapofika mbinguni tutashukuru Baba yetu kwa sababu hakuturuhusu kuendelea katika zambi, na tutafahamu ya kwamba kwa njia hii vilevile alionyesha wazi kabisa ya kwamba anatupenda.

# KRISTO

Sasa tutafundisha mambo matamu zaidi, habari za Bwana Yesu Kristo na kazi yake. Kristo alifunua Mungu kwetu, na baraka zote zinatufikia kwa njia yake. Mambo yaliyotokea zamani mbele ya kufa kwa Kristo yalitazamia kuja kwake. Baraka zote tutakazopata wakati wa kuja zitakuwa zetu kwa sababu ya mauti yake juu ya msalaba.

Tutagawa mafundisho ya Biblia juu ya Kristo kwa sehemu nane:

1. Uungu wake (Yeye ni Mungu)
2. Kazi yake mbele ya kuja kwake duniani
3. Kuja kwake kwa mwili wa mtu
4. Utu wake
5. Kazi yake hapa duniani
6. Kufa na ufufuko wake, na kurudi kwake mbinguni
7. Kazi yake sasa mbinguni
8. Kuja kwake mara ya pili.

## 1. KRISTO NI KWELI MWANA WA MUNGU?

Hili ni ulizo kubwa sana. *"Munafikili nini juu ya Kristo? Yeye ni Mwana wa nani?"* (Matayo 22:42). Kama Kristo ni kiumbe tu, hata akiwa kiumbe cha kwanza na kikubwa kuliko viumbe vyote vingine, imani ya Wakristo ni bule. Kwa sababu gani?

(1) Kwa sababu au Yeye au wanafunzi wake wangalikuwa wawongo.

(2) Kwa sababu mauti ya kiumbe kimoja haiwezi kulipa zambi za watu.

Biblia inafundisha kweli ya kama Kristo ni Mungu Mwana? Mwana ni sawasawa na Baba kwa kila njia? Alikuwa tangu zamani kama Baba?

Tumeona maneno kumi na mawili juu ya Mungu. Kumi ya maneno haya ni kweli juu ya Kristo vilevile. Maneno mawili ya kwanza tuliyosoma juu ya Mungu Baba yalikuwa ya kwamba Yeye ni Roho tu na watu hawawezi kumwona na macho. Maneno haya si kweli juu ya Mwana, kwani wakati alipokamata mwili wa mtu hapa duniani watu waliweza kumwona. Hakuwa tena Roho tu.

**Mwana wa Mungu ni wa milele** (Yoane 1:1). Katika mwanzo Neno alikuwa. Hakuwa na mwanzo. Alikuwa tangu zamani. Hata milioni ngapi za miaka zimepita tangu mwanzo, neno alikuwa mbele ya wakati ule. Shairi 14 la Yoane 1 linatufundisha ya kwamba "Neno" katika shairi 1 ni Kristo. Alishiriki utukufu wa Baba hata mbele ya kuumbwa kwa dunia (Yoane 17:5).

**Mwana wa Mungu ni juu ya mambo yote**, "wa kwanza katika yote" (Wakolosayi 1:18). Yeye ni sawasawa na Mungu kwa kila njia. Alisema hivi Yeye mwenyewe. *"Mimi na Baba yangu tu mmoja"* (Yoane 10:30). Mungu na Kristo tu wanaweza kusamehe zambi (Marko 2:5,7). Kristo aliruhusu watu kumwabudu namna ilivyowapasa kuabudu Mungu tu (Matayo 14:33), hata nyuma ya ufufuko wake toka wafu (Luka 24:52). Mwana wa Mungu ana ruhusa kufufua wafu na kuhukumu watu wote (Yoane 5:26-29). Watu wote watainama mbele yake (Wafilipi 2:10). Kiti chake cha ufalme ni cha milele na milele (Waebrania 1:8).

**Mwana wa Mungu anaweza kufanya maneno yote**. Katika Agano la Kale tunaona ya kwamba Mungu aliumba mbingu na dunia. Katika Agano Jipya tunaona alikuwa Mungu Mwana aliyeumba vitu vyote (Yoane 1:3; Wakolosayi 1:16; Waebrania 1:10).

Wakati alipokuwa hapa duniani, Mungu Mwana alikuwa na mamlaka juu ya upepo na bahari (Marko 4:39), juu ya pepo wachafu (Marko 5:8), na juu ya mauti (Marko 5:41). Alionyeshwa kuwa Mwana wa Mungu kwa uwezo (Waroma 1:4).

**Mwana wa Mungu anajua mambo yote** (Yoane 16:30; 21:17). Anajua mawazo ya watu (Matayo 9:4), hata wakati Yeye Mwenyewe si pamoja nao kwa pahali pamoja (Yoane 1:4-8). Anajua mambo yatakayotokea nyuma (Yoane 6:64; 13:3).

Mungu anajua mambo yote yatakayotokea nyuma na anakumbuka mambo yote yaliyokwisha kutokea. Anaweza kusahau vilevile kama akitaka. Kwa mfano, ameahidi kusahau zambi za wale walioamini Kristo (Waebrania 8:12).

**Mwana wa Mungu anaweza kuwa pahali pote kwa saa moja**. Kristo ni sasa kwa mkono wa kuume wa Mungu mbinguni na mwili wa mtu uliotukuzwa (Waefeso 1:20), lakini kila pahali waamini wawili au watatu wanapokusanyika pamoja kwa jina lake, Yeye ni pamoja nao kwa roho (Matayo 18:20). Ameahidi kuwa pamoja na wale wanaokwenda pahali pote duniani kuhubiri Habari Njema kama alivyoagiza (Matayo 28:19-20).

**Mwana wa Mungu amejifunua** (Yoane 2:11). Mungu ni nuru

(1 Yoane 1:5), na Kristo ni nuru ya dunia (Yoane 8:12). Mwana wa Mungu alikuja duniani ili kutufunulia Mungu. Yeye ni *"kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe"* (Waebrania 1:3).

**Mwana wa Mungu habadiliki** (Waebrania 1:12). *"Yesu Kristo ni sawasawa, jana, leo na hata milele"* (Waebrania 13:8). Neno kubwa zaidi lililotokea duniani lilikuwa kuja kwa Kristo kwa mwili wa mtu, Mungu na Mtu pamoja. Wakati Kristo alipofika hapa duniani kwa mwili wa mtu, hakuacha kuwa Mungu. Hakubadilika hata kidogo.

**Mwana wa Mungu ni Mwenye haki** (2 Timoteo 4:8). Anapenda haki na anachukia zambi (Waebrania 1:9).

**Mwana wa Mungu ni mtakatifu.** Malaika alimwambia Maria, *"Kile kitu kitakachozaliwa nawe kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"* (Luka 1:35). Wakristo wa zamani walioishi katika muda wa miaka mia moja ya kwanza nyuma ya mauti ya Kristo waliomba Mungu kwa jina la Mwana wake mtakatifu Yesu (Matendo 4:30).

**Mwana wa Mungu anajaa na neema** (2 Wakorinto 8:9). Alikuwa na huruma kwa watu (Matayo 9:36). Alipenda Kanisa na alijitoa kwa ajili yake (Waefeso 5:25). Sisi tunangojea rehema ya Bwana wakati atakapokuja kutupeleka kwake (Yuda 21).

Basi, tunaona kila kitu tulichosoma juu ya Mungu, tunakisoma juu ya Kristo vilevile. Si vizuri kusema Kristo anafanana na Mungu. Haifai kusema Kristo ni mwana wa Mungu namna sisi sote tulivyo wana wa Mungu. Kila mtu anayeamini mashairi tunayokwisha kuyasoma atafahamu ya kwamba Biblia inafundisha Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na zaidi ya ile, Yeye ni Mungu Mwana.

## 2. KAZI YA MWANA WA MUNGU MBELE YA KUJA KWAKE DUNIANI

Tumeona ya kama Mwana wa Mungu hakuwa na mwanzo. Alikuwa tangu zamani. Biblia inatupasha nini juu ya kazi yake mbele ya kuja kwake hapa duniani?

Neno moja linaloonyesha wazi ya kwamba Kristo ni Mungu ni uwezo ambao aliuonyesha wakati alipoumba ulimwengu. *"Ndani yake ulikuwa uzima"* (Yoane 1:4). Mungu aliumba ulimwengu kwa njia ya Mwana wake (Waebrania 1:2), na ndani yake vitu vyote vinashikamana (Wakolosayi 1:17).

Kazi kubwa ya pili ya Mwana wa Mungu mbele ya kuja kwake duniani ilikuwa kufunua Mungu kwa watu (Yoane 1:18). Shairi hili

linaonyesha ya kwamba wakati Mungu alipoonekana kwa watu wakati wa Agano la Kale, alikuwa Mungu Mwana. Mara nyingine alionekana kwa sura ya mtu, mara nyingine kwa sura ya malaika, mara nyingine kwa sura ya moto. Tunasoma Mungu alionekana kwa Abrahamu (Mwanzo 12:7), Isaka (Mwanzo 26:2), Yakobo (Mwanzo 35:9), Musa (Kutoka 3:2), Waisraeli (Walawi 9:4), Yosua (Yosua 5:13-15), Gideoni (Waamuzi 6:12), Manoa (Waamuzi 13:11), Samweli (1 Samweli 3:2l), Daudi (2 Mambo 3:1), Solomono (1 Wafalme 9:2), Isaya (Isaya 6:1), na Ezekieli (Ezekieli 1:28).

Neno la ajabu ndilo hili: Mungu alijifunua kwa njia ya Mwana wake. Kweli Yeye ni Mungu wa utukufu!

### 3. MWANA WA MUNGU ALIGEUKA MTU

Mwana wa Mungu alikuwa na ruhusa yote kukaa mbinguni. Tangu zamani alikuwa sawasawa na Baba yake. Aliweza kukaa pamoja na Mungu mbinguni kwa milele, kama akitaka. Lakini kama angalifanya hivi, watu wasingaliweza kuwa pamoja naye kamwe. Angalibaki peke yake kwa milele!

> *"Kama punza ya ngano isipoanguka kwa udongo na kufa, inakaa peke yake; lakini kama ikikufa, inazaa matunda mengi"* (Yoane 12:24).

Tumeona ya kwamba "Neno" katika sura ya kwanza ya Habari Njema ya Yoane ni Mwana wa Mungu.

> *"Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli"* (Yoane 1:14).

Katika Agano la Kale Mungu alitoa ahadi tena na tena ya kwamba siku nyingine Mwokozi atakuja atakayekuwa Mfalme.

Wakati Adamu na Hawa walipodanganywa na Shetani, ilipasa Mungu kuwahukumu. Lakini katika Mwanzo 3:15 aliahidi ya kwamba mtu mmoja atazaliwa na mwanamke atakayeharibu Shetani. Mwokozi atakuwa mtu aliyezaliwa na mwanamke.

Mungu alitoa ahadi tamu kwa Abrahamu kusema Mwokozi atakayeleta baraka kwa watu wote atazaliwa katika jamaa ya Abrahamu miaka mingi nyuma (Mwanzo 22:18). Alitoa ahadi hii kwa Isaka vilevile (Mwanzo 26:4), na kwa Yakobo (Mwanzo 28:14). Mungu aliahidi Yuda ya kwamba Mfalme huyu atazaliwa katika kabila lake (Mwanzo 49:10).

Mungu alionyesha ya kuwa Mwokozi huyu atakuwa Nabii kama Musa (Torati 18:15), Kuhani kama Melkisedeki (Zaburi 110:4), na

Mfalme atakayezaliwa katika jamaa ya Daudi (2 Samweli 7:16). Ilionekana wazi vilevile ya kwamba Mwokozi huyu hatakuwa malaika au kiumbe cha namna nyingine. Atakuwa mtu.

Mashairi mengine yanaonyesha ya kwamba Mungu Yeye Mwenyewe atakuja duniani.

> *"Katika siku ile itasemwa, Tazama, huyu ndiye Mungu wetu, ambaye tunamngojea, naye atatuokoa: huyu ndiye Bwana, tumemngojea; tutashangilia na tutafurahi katika wokovu wake"* (Isaya 25:9).
>
> *"Tazameni, Bwana Mungu atakuja"* (Isaya 40:10).

Yoane Mbatizaji aliagizwa kutengeneza njia ya Bwana na kunyolosha mapito kwa Mungu jangwani (Isaya 40:3; Yoane 1:23).

Malaki alitabiri,

> *"Bwana ambaye munamtafuta atakuja mbio hekaluni mwake"* (Malaki 3:1).

Isaya alitaja mengine ya majina ya Mfalme huyu atakayekuja:

> *"Mwenye ajabu, Mwenye shauri, Mungu Mwenye uwezo, Baba ya milele Mkubwa wa salama"* (Isaya 9:6-7).

Jina lake lingine ni Emanueli, maana yake "Mungu pamoja nasi." Alizaliwa na bikira (Isaya 7:14; Matayo 1:23). Hakuwa na baba aliyekuwa mtu wa dunia.

Namna gani Mfalme na Mwokozi huyu aliweza kuwa Mungu na Mtu pamoja? Tunapata jibu kwa ulizo hili katika Agano Jipya: Iliwezekana tu kwa njia ya Mungu kugeuka Mtu bila kuacha kuwa Mungu.

Katika Matayo 1 na Luka 2 tunasoma habari za kuzaliwa kwa Kristo na bikira. Ndani ya barua za Paulo kuna mashairi mengine yanayoonyesha wazi kabisa ya kwamba Yesu Kristo aligeuka Mtu.

> *"Na katika hawa alitoka Kristo . . . aliye juu ya maneno yote, MUNGU mbarikiwa kwa milele"* (Waroma 9:5).
>
> *"Mtu wa pili ni Bwana aliyetoka mbinguni"* (1 Wakorinto 15:47).
>
> *"MUNGU alionekana katika mwili"* (1 Timoteo 3:16).

Soma na waza juu ya mashairi haya vilevile: Wagalatia 4:4; Wafilipi 2:6-8; Waebrania 2:14.

Mwana wa Mungu aliye wa milele, asiyeumbwa, hakuacha kuwa Mungu wakati alipogeuka mtu. Ndiyo, hakuweza kuacha kuwa Mungu. Kweli ni ajabu kubwa kwa Mungu kutaka kugeuka mtu.

Aliweza kugeuka mtu kama akitaka. Alitaka kwa sababu anatupenda, na aliweza kwa sababu anaweza kufanya mambo yote.

### 4. UTU MKAMILIFU WA MWANA WA MUNGU

Hapa duniani Kristo alikuwa sawasawa na watu wote wengine, lakini hakuwa na tabia ya zambi.

(1) Ndiyo, mama yake alipata mimba kwa Roho Mtakatifu, si kwa mtu wa dunia (Matayo 1:20), lakini kwa njia zote nyingine kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa sawasawa na kuzaliwa kwa watoto wote. Waza sana juu ya Luka 1:31,35; 2:5-7,16,21,28.

(2) Ujana wake ulikuwa sawasawa na ujana wa watoto wengine (Luka 2:40-52). Aliuliza maneno. Alitii wazazi wake. Alipata nguvu katika mwili na katika akili, na katika neema mbele ya Mungu na watu.

(3) Kama watu wengine alisikia njaa (Matayo 4:2), alichoka (Yoane 4:6), na alipata kiu (Yoane 19:28). Hakutumia uwezo wake kama Mwana wa Mungu kamwe kwa kujisaidia Mwenyewe.

(4) Kama watu wengine alikuwa na mapendo (Marko 10:21), aliweza kukasirika (Marko 3:5), na kupata huzuni (Luka 13:34). Lakini hakuonyesha woga hata mara moja. Hata wakati alipokuwa katika hatari kubwa, aliamini Mungu na hakuogopa (Luka 4:29-30; Yoane 10:31-32).

(5) Mauti yake ilikuwa sawasawana mauti ya watu, lakini hakufa kwa sababu ya uzaifu. Alilia na sauti kubwa, kisha alitoa roho yake. "Ninatoa uzima wangu . . . hakuna mtu ambaye anauondoa kwangu" (Yoane 10:17-18). Wakati mtu anapokufa, mwili wake unatengwa na roho yake.

(6) Kama watu, Bwana Yesu Kristo alikuwa na nafsi (Matendo 2:31), roho (Luka 23:46), na mwili (Yoane 19:40).

Yesu Kristo alikuwa sawasawa na watu wote wengine ila katika jambo moja tu, ndilo zambi.

(1) Zambi ni kufanya neno ambalo Mungu alikukataza kufanya, na kukataa kufanya mambo ambayo alikuagiza. Kristo peke yake aliweza kusema,

> *"Sawasawa Baba yangu alivyonifundisha ninavyosema . . . ninafanya saa zote maneno ambayo yanampendeza"* (Yoane 8:28-29).

(2) Hata adui zake walilazimishwa kukubali sawasawa hakufanya neno baya hata moja.

*"Nani katikati yenu ambaye ananishitaki juu ya zambi?"* (Yoane 8:46).

Pilato alisema, *"Sioni neno baya kwake"* (Yoane 19:4,6).

(3) Mungu alionyesha toka mbinguni ya kama alipendezwa na Kristo:

*"huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ninapendezwa naye"* (Matayo 3:17; 17:5).

Zaidi ya mambo haya yote, Mungu alimfufua toka wafu. Neno hili linaonyesha kuliko maneno yote mengine ya kwamba kwa macho ya Mungu Mwana wake alikuwa mkamilifu. Hakufanya zambi (1 Petro 2:22). Ndiyo, hakujua zambi (2 Wakorinto 5:21).

**Kwa sababu gani utu mkamilifu wa Kristo ni neno kubwa?**

Tumeona ya kama Kristo alikuwa Mtu, Mtu mkamilifu. Kwa sababu gani neno hili ni neno kubwa?

Mtu tu aliweza kufunua Mungu kwa watu. Mtu tu anaweza kufa. Tunahitaji Mungu aliye Mtu vilevile kutuombea (1 Timoteo 2:5).

Sharti mtu ambaye atakufia watu awe mkamilifu yeye mwenyewe. Kama Yesu angalikuwa na zambi hata moja, ingalimpasa kufa kwa zambi yake Mwenyewe. Lakini Mwana-Kondoo ya Mungu alikuwa mkamilifu. Mwana wa Mungu alikuwa Mtu mzima, Mtu bila zambi, Mtu mkamilifu.

## 5. KAZI YA MWANA WA MUNGU HAPA DUNIANI

Mwana wa Mungu aligeuka Mtu pasipo kuacha kuwa Mungu. Hata wakati alipokuwa hapa duniani, alikuwa Mwana wa Mungu. Alionyesha utukufu wa Mungu, lakini hakutumika na uwezo wake wa Mungu kusaidia mahitaji yake mwenyewe. Ndani ya vitabu vya Habari Njema ya Matayo, Marko, Luka na Yoane tunasoma habari za maisha ya Yesu hapa duniani na kufa kwake.

Yesu aliishi karibu miaka 33 duniani. Habari nyingi ziliandikwa juu ya kuzaliwa kwake. Lakini kuna habari chache tu juu ya ujana wake kufika wakati alipokuwa na miaka 30. Habari hizi tunazisoma katika Luka 2:41-52. Vitabu vya Habari Njema vinatupasha zaidi juu ya miaka mitatu ya mwisho ya maisha yake.

**Kubatizwa kwake na Roho Mtakatifu** (Matayo 3:13-17; Marko 1:9-11; Luka 3:21-22). Wakati Yesu alipokuwa na miaka karibu 30, alibatizwa na Yoane katika mto Yorodani. Basi Yoane aliagiza watu kutubu kwanza, kisha aliwabatiza. Lakini Yesu

hakuwa na zambi ambazo alihitaji kutubu. Hata hivi alikubali kubatizwa kwa sababu watu wenye kupenda Mungu katika Israeli walikuwa wakibatizwa, naye alitaka kushiriki pamoja nao (Matayo 3:15).

Lakini Mungu hakutaka watu kufikili Yesu alikuwa akikiri zambi, hivi alimwita mara moja toka mbingu, "Mwana wangu, mpendwa wangu." Vilevile Roho Mtakatifu alimshukia kwa sura ya hua. Kristo alipewa Roho Mtakatifu pasipo kipimo (Yoane 3:34).

Katika Agano la Kale tunasoma juu ya makuhani (Kutoka 28:41) na wafalme (2 Samweli 2:4) waliopakaliwa na mafuta kwa mwanzo wa kazi yao. Mafuta ni mfano wa Roho Mtakatifu. Yesu alipakaliwa na Roho Mtakatifu. Alikuwa Masiya, ndiye "Yule aliyepakaliwa."

**Majaribu yake** (Matayo 4:1-11; Luka 4:1-13). Wakati Mungu alipoita Yesu "Mwana wangu, mpendwa wangu," alionyesha ya kwamba alipendezwa naye kwa utu wake. Basi Shetani alijaribu kuonyesha ya kama Yesu hataweza kukaa duniani bila kufanya zambi. Mungu alijua Mwana wake hatamkosea na hakuweza kumkosea. Shetani alijaribu na hila yote kuharibu mashauri ya Mungu, lakini alishindwa. Yesu hakufanya zambi.

**Maajabu yake**. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu Yesu aliponyesha wagonjwa, alisafisha wakoma, aliwezesha vipofu kuona tena, alifufua wafu, na alitoa pepo wachafu ndani ya watu (Luka 4:18; Matayo 12:28).

Kristo alifanya maajabu haya kwa sababu alipenda watu na alitaka kuwasaidia. Yalihakikisha vilevile ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Wakati watu walipofika kwake, aliwafundisha juu ya Mungu.

**Mafundisho yake**. Yesu hakuandika kitabu. Mafundisho yake yanapatikana ndani ya vitabu vine vya Habari Njema. Alifundisha watu juu ya Mungu Baba yake, juu ya ufalme wa mbingu na juu ya mauti yake mwenyewe, ufufuko wake na kuja kwake mara ya pili. Alihubiri Habari Njema waziwazi, lakini kweli nyingine za Mungu, za ndani ndani alizifundisha mara nyingi kwa njia ya mifano. Alikuwa na mafundisho mengine kwa wanafunzi wake tu.

## 6. MAUTI, UFUFUKO NA KURUDI KWAKE MBINGUNI

**Mauti yake**. Yesu alitendea watu wote mema. Kwa sababu gani viongozi vya Wayuda walimchukia? Walifikili mfalme atakayekuja

atakuwa mfalme mwenye utukufu mkubwa. Lakini Yesu alificha utukufu wake na alitumikia watu wengine (Marko 10:45). Wakati atakapokuja tena, atatawala na utukufu, lakini ilimpasa kuteswa kwanza.

Vilevile Yesu alihamakia watu juu ya zambi na kutokuamini. Alishitaki hata viongozi vyao kwa maneno ya Mungu, nao hawakupendezwa hata kidogo. Hivi taifa la Israeli waligeuka adui zake, wakaomba auawe.

Alishitakiwa mara mbili mbele ya wakubwa, lakini bila utaratibu na haki ya sheria, kwanza mbele ya wazee wa Wayuda, na mara ya pili mbele ya Pilato, liwali la Waroma. Halafu alihukumiwa kufa kwa njia ya kusulibishwa pamoja na wizi wawili. Rafiki zake walimwacha. Wayuda walimzarau, na askari walimtesa. Lakini alionyesha nini ilimhuzunisha kupita mambo haya yote wakati alipolia, "Mungu wangu, kwa nini umeniacha?" (Matayo 27:46).

Kwa sababu gani Mungu alimwacha? Kwa sababu "Yeye (Yesu) asiyejua zambi (Mungu) alimfanya kuwa zambi kwa ajili yetu" (2 Wakorinto 5:21). Wakati Mungu alipomfufua toka wafu alionyesha ya kwamba alikubali na kupokea sadaka ya Kristo kwa zambi.

**Ufufuko wake**. Wakati Yesu alipokufa, wale ambao walimpenda walifunga mwili wake na sanda na kumzika ndani ya kaburi lililochimbwa kilimani. Pilato na Wayuda waliagiza askari kusimama mbele ya kaburi hili na kulilinda ili wanafunzi wa Yesu wasipate njia kuiba mwili wake.

Lakini hata askari walilinda kaburi, siku ya kwanza ya juma kaburi hili lilionekana kuwa wazi bila maiti ndani. Yesu alikuwa hai tena na alijionyesha kwa Maria, wanawake wengine, Petro, wanafunzi wawili kwa kijiji Emau, wanafunzi kumi katika Yerusalema, Tomasi, waamini 500 pamoja kwa saa moja, Yakobo, wanafunzi saba kwa Galilaya, mitume yote, na Saulo karibu na Damasiki.

Saa yenyewe mwili wake ulikuwa mwili aliokuwa nao mbele ya kusulibishwa. Watu waliweza kuona vilonda ndani ya mikono yake na miguu yake. Alikula na kusemezana na wanafunzi wake. Lakini wakati alipotaka, aliweza kujificha kwao hata hawakuweza kumwona, na kutoka au kuingia mlango uliofungwa. Hakutumia uwezo huu mbele ya ufufuko wake.

**Kurudi kwake mbinguni.** Nyuma ya ufufuko wake toka wafu, Yesu alikuwa pamoja na wanafunzi wake wakati na wakati kwa muda wa siku 40. Aliendelea kuwafundisha juu ya Agano la Kale na Ufalme wa Mungu. Aliwaagiza kuhubiri Habari Njema pahali

pote duniani. Aliahidi kuwa pamoja nao siku zote na kutuma Roho Mtakatifu kwao nyuma ya siku chache. Halafu, wakati walipokuwa wakimtazama, alipanda kwenda mbinguni.

**Utukufu wake**. Alikuwa ametoka kwa Baba. Sasa alirudi karibu na Baba (Yoane 16:28). Alikuwa amekamata mwili wa mtu na kutii hata kufa. Kwa sababu hii Mungu alimtukuza sana, na kumpa jina lililo juu ya kila jina (Wafilipi 2:6-11). Mungu alimwikalisha vilevile kwa mkono wake wa kuume mbinguni na kuweka vitu vyote chini ya miguu yake (Waefeso 1:20-22).

## 7. KAZI YA KRISTO KWA WAKATI WA SASA

Wakati Yesu Kristo alipokwisha kumaliza kubeba azabu ya Mungu kwa zambi zetu juu ya msalaba, alilia na sauti kubwa, "Imekwisha" (Yoane 19:30). Halafu alikufa. Ni vizuri sana kwa mwenye zambi kutegemea kazi ambayo Kristo aliimaliza msalabani. Kwa njia hii tu anaweza kuokolewa.

Lakini kwa wenye zambi na kwa waamini vilevile ni vizuri kujua habari za kazi kubwa ambayo Kristo **hayamaliza** bado. Hatateswa tena kamwe kwa zambi zetu, lakini hata hivi ana kazi anayofanya kwa sisi hata sasa.

Kwa sababu Kristo ni Mungu na Mtu pamoja, anajua roho ya Mungu na roho za watu. Kweli tunahitaji mtu namna hii kusimama katikati yetu na Mungu. Ana majina matatu ambayo yanatufundisha juu ya kazi yake wakati wa sasa: MPATANISHI, KUHANI, MWOMBEZI.

**Mpatanishi** (1 Timoteo 2:5). Wakati Yobu alipotaabishwa sana, alifahamu ya kama alihitaji mwingine kusimama katikati yake na Mungu (Yobu 9:33). Kristo ni Mpatanishi mkamilifu kabisa. Alibeba gazabu ya haki ya Mungu ambayo ilitupasa sisi kuibeba. Wakati mtu anapoamini Kristo na kufa kwake kwa ajili yake, anapatanishwa karibu na Mungu, wala si adui yake tena.

Kristo ni Mpatanishi wa agano jipya lililo zuri zaidi (Waebrania 8:6; 9:15; 12:24). Kwa sababu ya neema ya Mungu tunapata faida ya agano hili. Kama Mpatanishi Kristo analeta kwa Mungu wapotevu walio na imani.

Kuna Mungu mmoja tu, na Mpatanishi mmoja. Tukisema tunahitaji mwingine, ni kama tunasema Kristo hatoshi. Ni vibaya sana kusema hivi. Hatuhitaji mwingine kusimama katikati yetu na Mungu. Yeye ni Mtu na anajua mioyo yetu. Hata hivi Yeye ni Mungu, na Mungu ni mapendo.

**Kuhani**. Ndani ya Agano la Kale tunasoma Mwokozi atakayekuja atakuwa Kuhani. Kristo ni Kuhani Mkubwa, mkubwa kuliko Haruni. Haruni na wana wake wote walikufa. Kristo ni Kuhani Mkubwa kwa milele. Melkisedeki ni mfano wake. Kazi ya kuhani mkubwa ni zaidi kuabudu na kuwaombea wengine (Waebrania 5:1-2). Kristo kama Kuhani wetu Mkubwa anaongoza kuabudu kwetu na anatengeneza sifa yetu kuwa kitu kinachoweza kukubaliwa na Mungu (Waebrania 10:19-22). Kama Kuhani, Yeye ni hai siku zote kutuombea, na hivi anaweza kuokoa kabisa watu wale wanaokuja kwa Mungu kwa njia yake (Waebrania 7:25).

**Mwombezi**. Mwombezi ni mtu anayesimamia na kuombea mtu mwingine. Kama *Mpatanishi* Kristo analeta wenye zambi kwa Mungu. Kama *Kuhani* anachunga waamini kwa pahali pa baraka. Lakini kama tukianguka kwa zambi, tunahitaji *Mwombezi*.

> *"Watoto wangu wadogo, ninawaandikia ninyi maneno haya ili musitende zambi. Na kama mtu akitenda zambi, tuna Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki"*
>
> (1 Yoane 2:1).

Shairi hili linatufundisha ya kwamba:

(1) Mungu hataki mimi kufanya zambi. (Lakini haifai kufikili tuko watu wakamilifu wasioweza kuanguka!)

(2) Wakati ninapofanya zambi hata hivi, nina Mwombezi, ndiye Yesu Kristo Mwenye haki. Kama mwana-sheria anavyojaribu kusaidia mtu kwa wakati wa matata, vivyo hivyo Kristo anatumika kurudisha karibu na Mungu tena mwamini yule aliyefanya zambi.

Kristo anaitwa na majina mawili mengine katika Agano Jipya yanayopasha juu ya kazi yake wakati wa sasa (1 Petro 2:25): MCHUNGAJI na MWANGALIZI.

**Mchungaji**. Kama Mchungaji Mwema Yesu alitoa uzima wake kwa ajili ya kondoo (Yoane 10:11). Kazi hii ilikwisha. Kama Mchungaji Mkubwa anatumika ndani yetu sasa kutukamilisha katika kila kazi njema sawasawa na mapenzi ya Mungu (Waebrania 13:20-21). Nyuma kidogo ataonekana katika utukufu na kuwapa zawabu wale ambao walimtumikia na uaminifu (1 Petro 5:4).

**Mwangalizi**. Mwangalizi ni mtu anayeangalia. Ni jina la Kristo kwa sababu anaangalia maneno ya makanisa na ya watu mmoja mmoja. Ni kazi yetu kumtumikia na uaminifu. Anawahamakia wale wanaotembea ovyo. Katika Ufunuo 2 na 3 tunaona ya kwamba anajua nini inafanyikana ndani ya makanisa. Anaahidi kuwapa zawabu

hata sasa wale ambao wanamtumikia na uaminifu, na zawabu kubwa zaidi kwa Kiti cha Hukumu cha Kristo wakati wa kuja. Lakini Yeye ni tayari vilevile kuondoa kinara cha kanisa walioacha njia ya Mungu na wanaokataa kutubu (Ufunuo 2:5).

## 8. KURUDI KWAKE MARA YA PILI

Tumeona ahadi za Mungu katika Agano la Kale ya kwamba Masiya, Nabii, Kuhani na Mfalme atakuja. Hapa duniani Bwana Yesu Kristo kama Nabii alijulisha watu mafikili ya Mungu. Sasa mbinguni, kama Kuhani, anatuombea. Nyuma kidogo atarudi kama Mfalme.

Hatarudi kama Mfalme wa Kanisa, lakini wa Israeli. Lakini wakati atakapokuja na utukufu, bibi arusi yake, ndilo Kanisa, litakuwa pamoja naye. Mbele ya mambo haya Kanisa litakutana na Bwana katika mawingu (1 Watesalonika 4:17), na kazi ya Wakristo itapimwa kwa kiti cha hukumu cha Kristo. Kisha Kristo atarudia dunia na utukufu na kusimamisha ufalme wake utakaoendelea kwa muda wa miaka elfu moja. Bwana Yesu ametukuzwa sasa mbinguni. Nyuma kidogo atatukuzwa duniani katikati ya watu vilevile.

# ROHO MTAKATIFU

Tumesoma mashairi machache ndani ya Biblia juu ya Mungu Baba na Mungu Mwana. Sasa tunataka kufundisha juu ya Mungu Roho Mtakatifu na kazi yake.

## 1. ROHO MTAKATIFU NI KAMA MTU

Watu wengine wanafikili Roho Mtakatifu ni kama pepo tu ambayo inatusukuma kutenda mema. Lakini ndani ya Biblia tunaona ya kwamba kwa njia nyingine Yeye ni kama mtu. Waza juu ya mashairi haya:

Mtu anaweza kusema, kutenda na kuonyesha mawazo yake. Roho Mtakatifu alisema, "Nilituma" na "Niliita" (Matendo 10:20; 13:2).

Mtu ana kutaka. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu. Ona 1 Wakorinto 12:11. Anashindana na watu (Mwanzo 6:3). Anaongoza wana wa Mungu (Waroma 8:14).

Mtu anasikia au furaha, au huzuni au mambo mengine kwa roho yake. Roho Mtakatifu anaweza kukasirika (Isaya 63:10). Anaweza kupata huzuni vilevile (Waefeso 4:30).

Mtu ana nia. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu (Waroma 8:27). Anatafuta mafumbo ya Mungu. Anajua maneno ya Mungu (1 Wakorinto 2:10-11).

## 2. UUNGU WA ROHO MTAKATIFU

Basi Roho Mtakatifu ni Mungu? Katika Biblia malaika wanaitwa roho, na wengine katikati yao ni roho watakatifu. Lakini tunaona wazi ya kama Roho Mtakatifu ni Mungu kama vile Kristo ni Mungu.

Maneno haya mawili "Roho Mtakatifu" (Luka 11:13) yanatufundisha maneno matatu: Yeye ni ROHO, na Yeye ni MTAKATIFU. Hatuwezi kumwona na macho kwani watu hawawezi kuona roho. Hivi kwa maneno haya matatu Roho Mtakatifu ni sawasawa na Mungu.

Yeye ni wa **milele** (Waebrania 9:14). Kila kiumbe ana mwanzo. Mungu tu ni wa milele.

Yeye ni **juu ya mambo yote,** na anaunganishwa pamoja na Mungu Baba na Mungu Mwana sawasawa (Matayo 28:19; 2 Wakorinto 13:14). Ingekuwa vibaya kuunganisha kiumbe hivi na Mungu.

Roho Mtakatifu anatoka kwa Baba na anatumwa na Mwana (Yoane 15:26; 16:7). Mtu akisema neno baya juu ya Kristo, anaweza kupata usamehe, lakini akifanya hivi na Roho Mtakatifu, hatasamehewa (Matayo 12:32).

Yeye ni **Mwenye uwezo wote**. Roho Mtakatifu alishiriki ndani ya kazi ya kuumba ulimwengu (Yobu 26:13). Kristo alifanya maajabu kwa uwezo wa Roho ya Mungu (Matayo 12:28).

**Anajua mambo yote**. Ona 1 Wakorinto 2:10.

Yeye ni **pahali pote wakati wote**. Ndani ya Zaburi 139:7-10 tunaona haiwezekani kukimbia Roho ya Mungu.

Yeye ni Mwenye haki. Anahamakia wasioamini juu ya zambi zao (Yoane 16:8-11).

Yeye ni **Mwenye neema**. Anaitwa Roho ya neema (Waebrania 10:29).

Mashairi haya yanaonyesha ya kuwa kumi ya maneno 12 tuliyosoma juu ya Mungu ni kweli juu ya Roho Mtakatifu vilevile. Yanatosha kuhakikisha Yeye ni Mungu. Maneno mawili mengine tuliyosoma juu ya Mungu ni ya kwamba anajifunua na ya kwamba habadiliki. Kabisa kabisa mambo yote tunayojua juu ya Mungu yanafunuliwa kwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Anaitwa Roho ya kweli (Yoane 14:17). Anajifunua (ndani ya Maandiko Matakatifu), lakini kazi yake kubwa zaidi ni kutukuza Kristo (Yoane 16:13-14). Kama Mungu, Roho Mtakatifu habadiliki kamwe.

Hivi tunaona Biblia inafundisha ya kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu.

## 3. KAZI YA ROHO MTAKATIFU

Sasa tunataka kuwaza juu ya kazi ya Roho Mtakatifu. Kuna Mungu mmoja tu, lakini anatumika kwa njia mbalimbali. Kazi ya Roho Mtakatifu haishindani na kazi ya Baba au ya Mwana. Kazi zao zote zinapatana vizuri. Ndani ya Biblia tunaona maneno saba yaliyo kazi ya Roho Mtakatifu.

### 1. Kuumbwa kwa dunia

Hata kama Mungu Mwana aliumba vitu vyote, Roho Mtakatifu alishiriki ndani ya kazi ya kuumba mtu (Yobu 33:4), na nyama (Zaburi 104:30). Alishiriki ndani ya kazi ya "kupamba" mbingu (Yobu 26:13), na ndani ya kutengeneza dunia tena (Mwanzo 1:2).

### 2. Kuandikwa kwa Biblia

Mafundisho makubwa ya Biblia ni juu ya Kristo, lakini ni

Mungu Roho Mtakatifu aliyeongoza waandishi na kuwaonyeshea nini iliwapasa kuandika (2 Petro 1:21).

**3. Wakati Kristo alipokuwa hapa duniani**

Tunaona kazi ya Roho Mtakatifu tena na tena ndani ya maisha ya Bwana Yesu Kristo wakati alipokuwa duniani.

*Kuzaliwa kwa Kristo*. Bikira Maria alipata mimba kwa Roho Mtakatifu (Matayo 1:18; Luka 1:35).

*Ubatizo wa Kristo*. Roho Mtakatifu alishukia Kristo nyuma ya ubatizo wake. Neno hili lilitimiza unabii katika Agano la Kale. Lilionyeshea Yoane na watu wengine ya kwamba Yesu Kristo alikuwa kweli Masiya. Lilionyesha vilevile ya kuwa Mungu alimkubali (Matayo 3:16-17; Marko 1:10-11; Luka 3:22).

*Majaribu ya Kristo*. Nyuma ya kubatizwa kwake Yesu aliongozwa na Roho Mtakatifu jangwani ajaribiwe na Shetani (Matayo 4:1; Marko 1:12; Luka 4:1).

*Utumishi wa Kristo*. Nyuma ya kushinda majaribu ya Shetani jangwani, Bwana Yesu Kristo alianza utumishi wake ulioendelea kwa miaka mitatu. Aliponyesha wagonjwa na kuhubiri Habari Njema kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Luka 4:14,18; Matayo 12:28).

*Mauti ya Kristo*. Bwana Yesu alikuwa na amri kutoa uzima wake kwa ajili ya kondoo, na kuutwaa tena. Alipokea agizo hili toka Baba yake (Yoane 10:18). Lakini tunasoma vilevile ya kwamba kwa Roho ya milele alijitoa Mwenyewe kwa Mungu, kuwa zabihu isiyo na kipaku (Waebrania 9:14).

*Ufufuko wa Kristo*. Katika Matendo 3:15 na mashairi mengine tunasoma Mungu alifufua Kristo toka wafu. Katika 1 Petro 3:18 tunasoma alifufuliwa kwa Roho Mtakatifu.

*Kurudi kwa Kristo*. Roho Mtakatifu anaamsha ndani ya bibi arusi (Kanisa) hamu kubwa kwa kurudi kwa Kristo (Ufunuo 22:17).

**4. Kazi ya Roho Mtakatifu kwa dunia**

Ni kazi ya Roho Mtakatifu kufahamisha watu wa dunia maneno ya zambi, ya haki, na ya hukumu (Yoane 16:8-11). Bila kazi ya Roho Mtakatifu watu hawawezi kufahamu ya kwamba wao ni wenye zambi.

***Kuna vizuizo viwili:***

(1) Mungu amewapa watu ruhusa kuchagua wao wenyewe

mambo wanayotaka. Halazimishi mtu kutenda yaliyo haki kama mtu mwenyewe asipotaka. Hivi Roho ya Mungu anazuizwa mara nyingine na hawezi kufanya kazi yake kwa sababu ya ukaidi wa mioyo ya watu, na mara nyingine mtu anafanya zambi isiyoweza kusamehewa, ndiyo kutukana Roho Mtakatifu (Matayo 12:32). Watu wanaweza kushindana na Roho Mtakatifu (Matendo 7:51), lakini haifai kufanya hivi. Mara nyingine wanatukana Roho ya neema (Waebrania 10:29).

(2) Lakini Roho Mtakatifu anazuiza vilevile. Anaweka mpaka kwa uadui na kuasi kwa watu hata zambi zisizidi kupita kipimo. Ataendelea kufanya hivi kufika siku atakapoondolewa duniani (2 Watesalonika 2:7). Halafu zambi na uasi zitazidi sana.

**5. Kazi yake ndani ya wale wanaotubu**

Ni kazi ya Roho Mtakatifu, kazi ya ajabu, kumpa kila mtu anayetubu na kuamini jina la Kristo, uzima wa Mungu (Yoane 3:5-6). Dakika ile ile mtu anazaliwa tena, na uzima ambao anaupata saa yenyewe utakuwa wake kwa milele na milele. Hautaondolewa kwake kamwe.

**6. Kazi yake ndani ya waamini**

Wakati unapozaliwa tena, unatakaswa, maana yake, unawekwa mbali kwa Mungu. Lakini zaidi ya neno hili unahitaji kutakaswa kila siku ungali hapa duniani. Hii ndiyo kazi ya Roho Mtakatifu (1 Petro 1:2), na ya Kristo (Waefeso 5:26).

Roho Mtakatifu anakaa ndani ya kila mwamini kufika siku ya kufa kwake (1 Yoane 2:27); anazaa matunda ndani yake (Wagalatia 5:22), na kumbatiza katika mwili wa Kristo (1 Wakorinto 12:13). Anataka kutujaza sisi sote mmoja mmoja (Waefeso 5:18), na ametutia mhuri kuonyesha sisi ni mali ya Mungu (Waefeso 1:13).

Lakini mtoto wa Mungu anaweza kuzuiza kazi hii nzuri ya Roho Mtakatifu. Inawezekana kwetu kuhuzunisha Roho Mtakatifu (Waefeso 4:30), au kumzima (1 Watesalonika 5:19), lakini ni vibaya kufanya hivi. Sharti makanisa wasikie sauti yake (Ufunuo 2:7,11,17,29; 3:6,13,22).

**7. Kazi yake ndani ya Kanisa**

Fikili kwanza juu ya ajabu hili: Watu wa mataifa na dini mbalimbali, matajiri na watu masikini, wote wanakutanishwa pamoja ndani ya mwili wa Kristo. Mmoja anakaa ndani ya watu hawa wote, ndiye Roho Mtakatifu. Anawapa uzima na kuwafanyiza kuwa moja ndani ya Kristo (1 Wakorinto 12:12-27).

# MALAIKA

Tumeona ya kwamba kweli zote zinapatikana ndani ya Biblia. Tumefahamu ya kuwa Biblia inatufundisha juu ya Mungu Baba, Kristo, na Roho Mtakatifu. Sasa tutaanza kujifunza juu ya viumbe Mungu alivyoumba. Mungu aliumba malaika, watu, na nyama.

Kwanza tufikili juu ya malaika, kuumbwa kwao, kuanguka kwao, kazi yao, na mwisho wao.

## KUUMBWA KWA MALAIKA

Malaika walitoka wapi? Ni viumbe vya namna gani? Malaika zote ni sawasawa?

Tumeona ya kwamba vitu vyote vilifanywa na "Neno la Mungu" (Yoane 1:3), ndiye Kristo. Paulo alisema, *"Katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo duniani, vitu vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni vitu vya wafalme au usultani au falme au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake"* (Wakolosayi 1:16).

Mwana wa Mungu aliumba malaika zote. Aliwaumba mbele ya kuumba ulimwengu na watu. Hatusomi ya kwamba Mungu aliumba tena malaika wengine nyuma.

**Hali** yao. Maana ya neno hili "malaika" kwa Kiebrania (lugha ya Agano la Kale) na kwa Kiyunani (lugha ya Agano Jipya) ni mtume. Ndani ya Agano la Kale neno lenyewe linatafsiriwa "mtume" mara nyingine na "malaika" mara nyingine.

Malaika wanaitwa "pepo" (Waebrania 1:7) na "roho" (Waebrania 1:14). Wengine wanaitwa "watakatifu" (Marko 8:38). Hawana mwili kama watu, hivi hatuwezi kuwaona. "Roho haina mwili na mifupa" (Luka 24:39). Mara nyingine malaika walionekana kwa watu kwa sura ya mtu kufanya mapenzi ya Mungu (Mwanzo 19:1,5). Hivi tunaona malaika ni roho ambao Mungu aliwaumba bila zambi, ili wamtumikie.

**Namna mbalimbali za malaika**. Ndani ya Biblia tunaona malaika ni namna mbalimbali.

(1) *Malaika mkubwa*, ndiye Mikaeli (Danieli 10:21; Yuda 9).

Malaika wengine tunaosoma majina yao ndani ya Biblia ni: Gabrieli (Danieli 8:16; Luka 1:19,26), na Lusifero.

(2) *Maserafi*. Tunawaona katika Isaya 6 tu, wakichunga kiti kitakatifu cha ufalme cha Mungu.

(3) *Makerubi*. Tunasoma juu yao kwanza katika Mwanzo 3:24 wakichunga njia ya mti wa uzima. Kulikuwa na mifano ya makerubi ndani ya Hema (Kutoka 25:18), ndani ya hekalu Solomono alilojenga (1 Wafalme 6:23), na kutakuwa na mifano ya makerubi vilevile ndani ya hekalu litakalojengwa kwa wakati wa kuja (Ezekieli 41:18).

(4) *Madaimoni* ni pepo wabaya (Waefeso 6:12). Bila shaka wao ndio malaika wale walioanguka ku zambi (2 Petro 2:4). Yuda anasema wengine wa malaika hawa ni katika vifungo (Yuda 6). Pepo hawa wabaya wanaoitwa pepo wachafu mara nyingine wanatumika na nguvu kujaribu kupanga ndani ya watu (Matayo 12:43-45).

## KUANGUKA KWA MALAIKA KWA ZAMBI

Pepo wabaya wanatoka wapi? Mungu aliumba vitu vyote kwa utukufu wake. Wengine wa viumbe vyake ni huru kufanya neno lo lote wanalotaka. Malaika na watu wanaweza kuchagua kufanya yaliyo mema au yaliyo mabaya.

Wengine wa viumbe hawa hawakuchagua vizuri na waliasi Mwumba wao. Kwa sababu hii Shetani ni ulimwenguni leo, na malaika walioanguka, na watu wenye zambi. Mungu hakuwaumba na hali hii.

Tunasoma mara mbili ndani ya Agano la Kale juu ya kuanguka kwa Shetani. Katika Isaya 14:12-20 nabii alitabiri kwanza juu ya mfalme wa Babeli (sh.4), na katika Ezekieli 28:11-19 juu ya mfalme wa Tiro. Lakini katika 28:2 Roho ya Mungu kwa njia ya Ezekieli anasema wazi na “mkubwa” wa Tiro. Hivi mashairi 11-19 yalisemwa na yule aliyeongoza mfalme huyu.

Bila shaka adui hawa za Waisraeli (Wababeli na watu wa Tiro) waliongozwa na kutawaliwa na Shetani. Ndani ya mashairi haya kwa Isaya na Ezekieli tunaona wafalme wa Babeli na Tiro kama mifano ya Shetani. Maneno mengine tunayosoma juu yao hayawezi kutimizwa na mtu tu. (Tunaona neno hili vilevile ndani ya mashairi mengine yanayopasha kwanza juu ya mtu wa Mungu, lakini wakati tunapoangalia mashairi haya karibu karibu, tunaona yanapasha juu ya Kristo.)

Tuone sasa mambo mengine juu ya Shetani. Aliitwa Lusifero (Isaya 14:12). Alikuwa na pahali pa heshima, mwenye akili nyingi, na mwenye kuonekana vizuri sana (Ezekieli 28:12-15). Alipewa ruhusa kutawala sehemu ya ulimwengu.

Wakati Lusifero alipoanza kuwa na kiburi zambi iliingia dunia hii Mungu aliyoumba. Alisema, *"Nitapanda mbinguni, nitanyanyua kiti changu cha ufalme juu kuliko nyota za Mungu, na nitakaa juu ya mlima wa makutano . . . nitafanana na Mjuu Sana"* (Isaya 14:13-14). Ndiyo, alitaka kuwa sawasawa na Mungu!

Malaika wengi walifungana pamoja na Shetani na walianguka pamoja naye. Walifukuzwa mara moja toka pahali Mungu alipo, kwani Mungu hawezi kuvumilia zambi hata kwa dakika moja. Hawajahukumiwa bado, lakini watahukumiwa bila shaka kwa wakati wa kuja (Isaya 14:12,15; Ufunuo 12:4,9).

## KAZI YA MALAIKA

Tumeona ndani ya Biblia ya kwamba malaika waliumbwa na Mungu. Tumeona wengine, walioongozwa na Lusifero, waliasi Mungu. Sasa tuwaze juu ya kazi yao wakati wa sasa, na nini itawapata kwa wakati wa kuja, malaika wema na malaika wabaya.

### 1. Malaika wabaya

Malaika wabaya wanafanya nini sasa? Ndani ya Biblia tunapata habari nyingi juu ya Shetani na habari chache juu ya pepo wachafu na malaika watakatifu.

**Shetani**. Tuwaze kwanza juu ya majina ya Shetani.

(1) *Lusifero* lilikuwa jina la Shetani mbele ya kuanguka kwake. Ona tena sura uliyomaliza kuisoma sasa tu.

(2) *Nyoka*. Katika Mwanzo 3:1,4 nyoka alisema uwongo na Hawa. Katika Mwanzo 4 Kaina aliyekuwa "wa yule mwovu" (1 Yoane 3:12), aliua ndugu yake. Hivi hatushangai kuona Bwana Yesu Kristo akiita Shetani mwuaji tangu mwanzo na baba ya wongo (Yoane 8:4-44). Hivi jina hili la Shetani, "Nyoka," linatukumbusha udanganyifu na kuchukia kwake.

(3) *Shetani*. Maana ya neno hili ni "adui", kama katika Zekaria 3:1. Shetani ni adui kweli ya Mungu na watu wake. Mara nyingine anashindana nao waziwazi. Saa yenyewe anazungukazunguka kama simba ya kunguruma, akitafuta mtu ammeze (1 Petro 5:8). Mara nyingine anaonekana kama malaika ya nuru (2 Wakorinto 11:14). Kuchukia kwake kwa Kristo hakuwezi kupunguka.

(4) *Yule mwovu* ni jina lingine la Shetani. Ananyanganya mbegu njema (Matayo 13:19) na anapanda mbegu mbaya (13:28, 38). Anatupia watakatifu mishale ya moto, lakini wanaweza kuzima mishale hii kwa njia ya imani (Waefeso 6:16). Hata waamini wa sasa tu wanaweza kushinda Shetani na kujichunga wenyewe hata Shetani asiweze kuwaumiza (1 Yoane 2:13).

(5 ) *Diabolo*. Maana ya neno hili ni "mshitaki". Shetani anafanya mashitaki yake kwa njia ine.

*Anashitaki watu kwa Mungu*. Kwa mfano, alisema Yobu alitumikia Mungu kwa sababu ni faida kwa yeye mwenyewe, si kwa sababu alitaka kupendeza Mungu. Anashitaki Wakristo mbele ya Mungu mchana na usiku (Ufunuo 12:10).

*Anashitaki Mungu mbele ya malaika za mbingu* (Yobu 1:6,10). Alisema Mungu alikuwa na upendeleo kwa Yobu. Neno hili ni neno kubwa. Unakumbuka ya kwamba Mungu alifukuza Shetani na malaika wengi wengine toka mbinguni kwa sababu ya zambi zao. Shetani anasema wakati Mungu alipofanya hivi hakutenda kwa haki. Anasema vilevile Mungu hatendi kwa haki kwa sababu hahukumu zambi za watu mara moja. Moja la makusudi makubwa ya kuumbwa kwa dunia na ukombozi wa watu ni kwa Mungu kunyamazisha kwa milele mashitaki ya Shetani ya kwamba Yeye ni mzalimu.

*Anashitaki Mungu kwa watu*. Maana ya maneno yake katika Mwanzo 3:5 ni kusema Mungu ni mwenye wivu, mwenye kujifikili mwenyewe tu, na kwa sababu hii hakutaka Adamu na Hawa kula matunda ya mti wa kujua uzuri na ubaya. Shetani anataka kuingiza ndani ya roho zetu shaka juu ya mapendo ya Mungu. Watu wanasema ni vibaya kwa Mungu kuacha watu kuteswa. Ni Shetani anayeweka mawazo kama haya ndani ya nia zao.

Shetani *anatushitaki kwa wenzetu*. Kwa mfano alijaribu kuleta kutokufahamana katikati ya Paulo na Wakorinto (2 Wakorinto 2:11), lakini Paulo alijua desturi yake na hila yake.

(6) *Mjaribu* (Matayo 4:3). Shetani alishinda wakati alipojaribu Adamu na Hawa. Aliwajaribu kwa njia ya tamaa ya mwili (mzuri kwa chakula), tamaa ya macho (ulipendeza macho), na kiburi cha uzima (mti wa kutamaaniwa, Mwanzo 3:6). Yoane alisema mambo haya matatu hayatoki kwa Mungu Baba (1 Yoane 2:16). Alisema kweli kabisa.

Adamu na Hawa walianguka kwa zambi. Basi Shetani alijaribu kuangusha Bwana Yesu Kristo vivi hivi, lakini alishindwa (Matayo

4:1-11). Alisema na Yesu, *"Amuru mawe haya yawe mikate"* (tamaa ya mwili). Halafu alisema, *"Haya yote nitakupa"* (tamaa ya macho). Mwishoni alisema, *"Kama ukiwa Mwana wa Mungu, ujitupe mwenyewe chini"* (kiburi cha uzima).

**Pepo wachafu**. Watu wengine wanafikili Shetani anajua maneno yote na ana uwezo wote kama Mungu. Lakini sivyo. Shetani hawezi kuwa pahali pote saa moja. Sharti afanye kazi yake kwa njia ya pepo wachafu wengi ambao wanaomtii. Pepo wabaya hawa ndio miungu ya wapagano (1 Wakorinto 10:20). Wanaitwa mashetani hapa. Ni vilevile roho za manabii wa uwongo. Kwa njia nyingine uwezo wao unapita uwezo wa watu (Torati 13:1-3; Matayo 24:24; Ufunuo 13:13-15).

**2. Malaika watakatifu**

Malaika watakatifu ndio wale wasioanguka kwa zambi. Wanafanya kazi gani?

**Kwa wakati wa zamani**, walichunga kiti cha ufalme cha Mungu (Mwanzo 3:24; Isaya 6:2). Kama wajumbe walitumwa mara nyingi kujulisha watu mapendo ya Mungu au kuleta hukumu yake juu yao (Mwanzo 19:1,13). Malaika walisaidia ndani ya kazi ya kuleta Sheria (Wagalatia 3:19; Waebrania 2:2).

**Kwa wakati wa sasa**, wao ni "roho za kutumikia, waliotumwa kutumikia wale watakaoriti wokovu" (Waebrania 1:14). Kwa mfano, malaika waliponyesha Petro toka gereza (Matendo 5:19; 12:7).

Wanapenda sana kutazama namna Mungu anavyotutendea sisi kwa hekima na neema kubwa (Waefeso 3:10; 1 Petro 1:12).

**Kwa wakati wa kuja** wataleta gazabu ya Mungu itakayopata waasi (2 Watesalonika 1:7; Ufunuo 8:2; 16:1).

**3. Nini itapata malaika wakati wa mwisho?**

Wengine wa malaika walioanguka kwa zambi ni hata sasa katika vifungo wakingoja siku ya hukumu. Wengine wengi watahukumiwa na kupata azabu yao wakati wa kuja.

Kama katika Yobu 1, Shetani anaweza kutokea mbele ya kiti cha ufalme cha Mungu hata sasa (Ufunuo 12:10). Kwa wakati wa sasa yeye ni mkubwa wa "watawala wa ulimwengu wa giza hili . . . katika pahali pa mbingu" (Waefeso 6:12). Atatupwa chini hata dunia wakati wa Mateso Makubwa (Ufunuo 12:9). Halafu atafungwa ndani ya shimo linalokwenda chini sana kwa miaka elfu moja

wakati Kristo anapotawala hapa duniani (Ufunuo 20:2-3), kisha atafunguliwa tena kwa muda mfupi. Ataongoza watu wa dunia mara ya mwisho kuasi Mungu, lakini watashindwa. Halafu atatupwa ndani ya ziwa la moto lililotayarishwa kwa yeye na malaika zake. Pale atateswa kwa milele na milele (Ufunuo 20:7-10).

Malaika watakatifu watatumikia Mungu (Ufunuo 21:12), na kufurahi kwa milele wakitazama ufunuo wa neema yake (Waefeso 2:7).

# MTU

Viumbe vingine vilivyoumbwa na Mungu ni watu. Malaika waliumbwa kwanza na wanapita watu kwa njia nyingine. Biblia inafundisha nini juu ya watu na makusudi ya Mungu juu yao?

**1. Mwanzo wa mtu**

Watu wasingaliweza kujua pahali walipotoka isipokuwa Mungu aliwaambia habari hizi. Kwa sababu Mungu ni Mwenye neema, alitujulisha mambo haya makubwa katika Mwanzo 2:7.

Mungu aliumba mtu namna gani? Alifanya mwili wake toka mavumbi ya inchi. Vitu vilivyo ndani ya mwili wa mtu ni sawasawa na vile vinavyopatikana ndani ya nyama na vitu vingine kama mawe, mapando na vingine

Halafu Mungu alifulisha pumzi ya uzima ndani ya pua ya mtu naye alipata uzima. Hata leo watu hawafahamu kama uzima ni nini na hawawezi kufanyiza kitu kisicho na uzima kuwa kitu hai.

Hata kama watu wengine wakiamini mafundisho ya évolution, kuna mambo mengine évolution isiyoweza kueleza. Haiwezi kuonyesha namna gani mapando yalianza kuota duniani, mwanzo wa nyama na mwanzo wa watu.

Mtu wa kwanza aliumbwa wakati gani? Biblia inafundisha ya kwamba Adamu alikuwa mtu wa kwanza. Miaka karibu elfu saba imepita tangu Mungu alipomwumba. Walimu wa Evolution wanasema wamepata udongoni mifupa ya watu na vitu vilivyofanywa na watu vilivyo vizee kupita miaka elfu saba. Labda kulikuwa na viumbe **vilivyoonekana** kama watu hata mbele ya kuumbwa kwa Adamu. Lakini Adamu aliumbwa na roho. Hakuna njia kuhakikisha ya kwamba viumbe hivi vya zamani (kama kweli kulikuwa na viumbe namna hii) vilikuwa na roho. Hivi mifupa hii haiwezi kuhakikisha ya kwamba habari tunazopata ndani ya Biblia juu ya kuumbwa kwa mtu si kweli.

**2. Cheo cha mtu**

Katika Zaburi 8 tunaona ya kwamba mtu alifanywa chini kupita malaika (sh.5), na juu kupita nyama (mash.6-8). Hata katikati ya watu kuna tofauti: “Kichwa cha mwanamume ni Kristo; kichwa cha

mwanamke ni mwanamume; na kichwa cha Kristo ni Mungu" (1 Wakorinto 11:3). Sharti watu watii wafalme na watawala (1 Petro 2:13-14; Waroma 13:1). Yesu ni juu ya viumbe vyote (Waebrania 2:6-9; Ufunuo 3:14).

**3. Hali ya mtu**

Mtu ana mwili, nafsi na roho (1 Watesalonika 5:23).

Mwili wake ndio nyama, mifupa na damu. Malaika hawana mwili.

Kwa wakati wa sasa mwili unaweza kupatwa na ugonjwa na kufa. Wakati Kristo atakapokuja, Wakristo watapata mwili mpya utakaokuwa sawasawa na mwili wake (1 Wakorinto 15:53; 1 Yoane 3:2).

Kwa sababu Mungu alifufua Bwana Yesu Kristo toka wafu, tunaweza kujua bila shaka ya kuwa watu wote watafufuliwa vilevile. Lakini ni huzuni kufikili ya kwamba waovu watafufuliwa kwa kuhukumiwa kwa zambi zao (Yoane 5:28-29).

Mtu ana nafsi vilevile. Na nafsi yake anafikili, anasikia furaha au huzuni, na anafahamu kitu anachotaka. Kuna mashairi mengine ndani ya Biblia yanayoonyesha wazi ya kuwa nafsi na roho si kitu kimoja. Ona Waebrania 4:12. Basi roho ya mtu ni nini?

Roho ya mtu inamwezesha kuwa na upatano na Mungu aliye Roho. Mtu ni namna nyingine na nyama kwa sababu ana roho, kitu nyama asichokuwa nacho. Nyama hawezi kuwa na upatano na Mungu.

Zamiri ya mtu ni sehemu ya roho yake. Inawezekana kwa nyama kuogopa azabu, lakini hajui kitu gani ni kizuri na kitu gani ni kibaya. Zamiri ni kama kiongozi ndani ya mtu. Inamwongoza kwa kipimo anachojua mambo gani ni mambo mazuri au mabaya. Kwa mtu aliyejifunza uzuri na ubaya ndani ya Biblia, ni vizuri sana kuwa na zamiri safi, zamiri ambayo haimshitaki juu ya zambi kwa sababu hakufanya zambi. Lakini mtu akiwa na zamiri mbaya na akifunga masikio yake kwa sauti ya zamiri ndani yake, nyuma ya wakati zamiri haitamchokoza tena.

Wakati mtu anapokombolewa, anaokolewa mzima — mwili wake (Waroma 8:23), nafsi yake (1 Petro 1:9), na roho yake (Waebrania 12:23).

**4. Uwezo wa kuchagua**

Mungu ameumba mtu kwa sura yake mwenyewe na amempa uwezo kuchagua kwa yeye mwenyewe. Hivi mtu anaweza kucha-

gua kutenda mema au mabaya. Lakini hata hivi yeye si huru kabisa kwa sababu inampasa kutii sheria za inchi pahali anapoishi.

Kwa maneno ya Mungu vilevile mtu ni huru kuchagua uzuri au ubaya, kutenda yaliyo mema au maovu. Tumeona neno hili ndani ya shamba la Edeni. Mungu alikataza Adamu neno moja, hivi Adamu alijua mara moja nini ni vizuri na nini ni vibaya.

**5. Mungu aliumba mtu kwa sababu gani?**

Mungu ni mapendo (1 Yoane 4:8). Aliumba mtu aweze kumpenda, na mtu aweze kumpenda Yeye Mungu vilevile.

Shetani aliongoza mtu kufanya zambi kwa sababu alitaka kuharibu makusudi ya Mungu. Labda alifikili kama Mungu akiazibu mtu kwa zambi zake, mtu hatampenda, lakini atamchukia. Inatokea hivi mara nyingi. Lakini kwa sababu ya zambi Mungu alipata njia kuonyesha mapendo yake kwa mtu hata kupita mbele. Hivi mashitaki ya Shetani kwa Mungu yatanyamazishwa kwa milele. Kristo atakuwa na jeshi kubwa la wakombolewa pamoja naye mbinguni. Watampenda kwa sababu Yeye aliwapenda kwanza (1 Yoane 4:19). Utakuwa mmoja wao?

**6. Mungu anataka mtu kufanya nini?**

Kusudi kubwa la Mungu Baba ni kutukuza Mwana wake, Bwana Yesu Kristo. Aliumba mtu kwa kusudi hili tu. Anataka mtu kujifunza mapenzi ya Mungu na kuyafanya. Anataka vilevile mtu kutumia kutaka kwake kwa utukufu wa Mungu na kuleta utukufu na heshima kwa Mwana wa Mungu.

**7. Kuanguka kwa mtu**

Soma juu ya MWANZO WA ZAMBI kwa ukurasa 47.

# WOKOVU

Sura sita zinazofuata zinaeleza mafundisho ya Biblia juu ya wokovu.

## HITAJI LA WOKOVU

Neno fupi moja linatuonyeshea hitaji letu kwa wokovu. Neno hili ni ZAMBI. Kama zambi isipokuwa, kama tusingalihitaji wokovu. Tuone nini Biblia inayofundisha juu ya zambi, namna gani iliingia duniani, na matunda yake.

### 1. Mwanzo wa zambi

Zambi iliingia ulimwengu wakati gani na pahali gani? Mungu aliumba zambi? Aliumba viumbe vyenye zambi?

**Shetani**. Mungu aliumba viumbe wanaoweza kumpenda na kumtumikia kwa sababu wao wenyewe wanataka hivi. Wanaweza kumchukia vilevile na kumwasi. Kuasi Mungu ni zambi. Kama viumbe hawa wasingaliweza kufanya zambi, ingalikuwa sharti kwao kutii. Lakini Mungu hakuumba watu hivi. Alitaka wawe huru kuchagua au kumtii au kumwasi. Hivi wengine walichagua kumwasi. Wa kwanza alikuwa Lusifero. Wakati wa nyuma Lusifero aliitwa Shetani.

**Mtu**. Unaweza kusoma habari za zambi za Adamu katika Mwanzo 3. Waza juu ya mambo haya:

(1) Ndani ya Shamba la Edeni kila kitu kilitengenezwa kusaidia mtu kukaa na furaha. Aliweza kula matunda ya miti iliyokwisha kupandwa mbele. Alikuwa mtawala wa nyama zote. (Kwa masawanisho Bwana Yesu Kristo anayeitwa vilevile Adamu ya mwisho alijaribiwa nyuma ya kushinda siku makumi ine jangwani bila kula chakula.)

Adamu alisemezana na Mungu kila siku shambani mwa Edeni. Alikatazwa kitu kimoja tu. Hakuweza kula matunda ya mti wa kujua uzuri na ubaya.

(2) Mungu alisema na Adamu waziwazi ya kwamba siku atakapoasi agizo hili atakufa. Hivi Adamu hakuweza kutoa uzuru kusema hakujua.

(3) Wakati Shetani alipotaka kujaribu Adamu kufanya zambi, alifika kwanza karibu na Hawa. Alisema naye neno lililoamsha shaka rohoni mwake juu ya wema wa Mungu. Hawa alisema uwo-

ngo wa kwanza. Alimwambia Shetani hawana ruhusa kugusa mti wa kujua uzuri na ubaya. Lakini Mungu hakuwakataza kugusa mti huu. Aliwakataza tu KULA matunda yake. Kama wakikula watakufa.

Halafu Shetani alisema wazi hata wakikula matunda ya mti hawatakufa. Aliahidi kwa Hawa ya kwamba watakuwa sawasawa na Mungu na kujua uzuri na ubaya. Hawa aliamini uwongo wa Shetani, basi alidanganywa. Zambi ya Adamu ilikuwa kubwa kupita ile ya Hawa kwa sababu hakudanganywa (1 Timoteo 2:14).

(4) Ahadi ya Shetani ilitimizwa? Basi hata mbele ya kula tunda la mti huu Adamu na Hawa walijua nini ni vizuri na nini ni vibaya. Walijua tangu dakika ile wakati Mungu alipowakataza kula matunda. Lakini sasa walijua ubaya kwa njia ya kuufanya wao wenyewe.

(5) Mungu alisema nao mbele ya kwamba siku watakapoasi agizo lake, watakufa. Neno hili lilifanyikana kweli?

Siku ile ile wakati Adamu alipoanguka kwa zambi alitengwa na Mungu. Kutengwa na Mungu ni kufa. Vilevile bila shaka mwili wa Adamu ulianza kufa siku yenyewe. *"Mshahara wa zambi ni mauti"* (Waroma 6:23). Lakini zambi ni nini?

**2. Zambi ni nini?**

Kwa watu wengine zambi ni furaha za dunia. Watu wengine wanafikili zambi ni kama ugonjwa. Wengine wanasema hakuna zambi. Wengine wanafikili zambi ni kufanya mambo yasiyo haki, lakini ya kwamba hatuwezi kujizuiza tusifanye mambo haya.

Mungu ana ruhusa kuniagiza maneno anayotaka niyafanye na kunikataza maneno mengine, na amefanya hivi. Nikifanya maneno ambayo Mungu ananikataza kufanya, ninafanya zambi. Kama nikikataa kufanya maneno ambayo Mungu ananiagiza kufanya, au nikisahau kuyafanya, ninaanguka vilevile. "Zambi ni uasi" (1 Yoane 3:4). Ni kuvunja Sheria ya Mungu. Hata nisipojua Sheria ya Mungu, ninakosa wakati ninapoivunja. Lakini nikijua kutenda mema wala siyatendi, hii ni zambi vilevile (Yakobo 4:17).

*"Yote yasiyo ya haki ni zambi"* (1 Yoane 5:17).

*"Fikili la mpumbavu ni zambi" (*Mezali 24:9).

*"Kila tendo lisilotoka katika imani ni zambi" (Waroma 14:23).*

Au, kwa ufupi, zambi ni kuasi Mungu. Ni kusema, "Nitafanya neno MIMI ninalotaka kufanya, si neno kama MUNGU akitaka nini."

Lakini zambi ni kama bwana mkali ya kazi.

*"Kila mtu anayefanya zambi ni mtumwa wa zambi"*

(Yoane 8:34).

Zambi ni udanganyifu (Waebrania 3:13).

Zambi inaleta mauti (Yakobo 1:15).

MUNGU ANACHUKIA ZAMBI (Yeremia 44:4). Anakasirikia waovu kila siku (Zaburi 7:11).

Zambi gani ni zambi kubwa zaidi? Zambi namna namna zinatajwa pahali mbalimbali ndani ya Biblia. Katika Matayo 15:19 zambi inayotajwa kwanza ni "mawazo mabaya". Katika Wagalatia 5:19 ni uasherati. Katika Marko 7:22 kiburi na upumbavu zinatajwa kwa mwisho. Ndani ya Waroma 1:29-30 zambi za kusingizia watu na kuasi wazazi zinatajwa vilevile.

Labda kiburi ni zambi mbaya zaidi. "Kuna maneno sita ambayo Bwana anayachukia, ndiyo, saba yaliyo machukizo kwake: macho ya kiburi . . ." (Mezali 6:16). Ni zambi ya kiburi inayozuiza watu wengi wasifike karibu na Mungu kupata wokovu, kwani kiburi inawazuiza wasikiri zambi zao. Lakini Mungu anaokoa wenye zambi tu, si watu wale wanaofikili wao ni watu wazuri na wenye haki (Luka 5:32). Anaweza kusaidia watu kwa njia ya Kristo tu. Kukataa kupokea Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wako ni zambi isiyoweza kusamehewa. Ni tunda la kiburi na roho ya uasi.

**3. Matunda ya zambi**

Mtu akiasi Mungu anatenda zambi. Basi zambi hii inazaa matunda gani kwa Mungu, Shetani, na watu?

**Kwa Mungu**: Kwa sababu mtu alikosea Mungu, inapasa Mungu kumwazibu. Mungu ni Mwenye haki. Hawezi kuvumilia waasi karibu naye. Kama mwasi asipotubu, sharti akae mbali na Mungu kwa milele.

Lakini Mungu ni mapendo vilevile. Mapendo yake kwa watu hayawezi kugeuka. Anawataka wale ambao anawapenda kuwa pamoja naye. Hivi tunaona haki ya Mungu ikifukuza watu, na mapendo yake yakiwakokota karibu. Basi mwisho wake nini?

Usifikili neno hili liliweza kufazaisha au kushinda Mungu. Alijua tangu mwanzo maneno yatakayotokea. Hivi alitengeneza njia ya ajabu kurudisha watu karibu naye. Ndiyo, zambi iliingia duniani, lakini haikuweza kuzuiza Mungu kuwa mwenye haki au Mwenye mapendo. Na kwa msalaba wa Kristo tunaona mapendo NA haki ya Mungu wazi kuliko pahali po pote pengine.

**Kwa Shetani**: Kwa sababu ya zambi ya watu Shetani alipata njia kushitaki Mungu na watu. Mtu alifungulia adui ya Mungu njia kumtukana (2 Samweli 12:14). Lakini mashitaki haya yote yatanyamazishwa kwa milele kwa njia ya kazi ya Kristo.

**Kwa mtu**: Tunda la kwanza la zambi kwa mtu lilikuwa woga. Adamu na Hawa walianza kuogopa Mungu. Kwa mwanzo walisemezana na Mungu kila siku, lakini nyuma ya kufanya zambi walijaribu kujificha wasione Mungu tena. Walijua walikuwa watupu na waliogopa kufika mbele yake (Mwanzo 3:8).

Vilevile Mungu hakuweza kuwaruhusu kuwa karibu naye tena. Hivi tunda la pili la zambi yao lilikuwa kufukuzwa kwenda mbali na Mungu. Watu ni "wafu kwa sababu ya makosa na zambi" (Waefeso 2:1).

Wakati mtu alipofanya zambi alijiweka chini ya utawala wa Shetani. Kwa sababu anaogopa mauti, yeye ni mtumwa (Waebrania 2:14-15). Alifikili atakuwa sawasawa na Mungu na KUJUA, lakini macho yake yalipofushwa na Shetani (2 Wakorinto 4:4).

Kwa sababu Adamu aligeuka mwenye zambi, watu wote wanaozaliwa kwa njia yake wanazaliwa na tabia ya zambi na ni nyepesi kwao kutenda zambi. Siku nyingine Mungu atauliza kila mtu juu ya matendo yake yote.

## MSINGI WA WOKOVU

Mungu alitaka kuokoa watu toka matunda ya zambi. Bila shaka watu wanahitaji kuokolewa. Lakini Mungu ataweza kuwaokoa namna gani?

Kwa ufupi, Mungu anaweza kuokoa watu kwa sababu ya kufa kwa Bwana Yesu Kristo msalabani. Kutusaidia kufahamu ukubwa wa maneno haya, tufikili maneno mane:

### 1. Kipatanisho

Mungu anachukia zambi na akiwa Mwamuzi anaonyesha gazabu yake ya haki kwa mwenye zambi. Lakini anapenda mwenye zambi vilevile. Baba anapenda mwana wake hata wakati anapomwazibu kwa sababu ya kuasi kwake. Mara nyingine inapasa mwamuzi kuhukumu hata mwana wake mwenyewe. Mungu kama Mwamuzi hawezi kuwa na upendeleo.

Neno la kwanza tunalotaka kufikili juu yake ni KIPATANISHO. Gazabu ya Mungu inatulizwa kwa njia ya sadaka. Kwa sababu

Bwana Yesu Kristo alibeba azabu ya zambi zetu wakati alipojitoa kama sadaka kwa Mungu juu ya msalaba, Mungu hahitaji kuwa na gazabu kwa mwenye zambi tena. Anaweza sasa kumwonyeshea rehema yake.

Mungu "akatuma Mwana wake kuwa kipatanisho kwa zambi zetu" (1 Yoane 4:10).

*"Naye ni kipatanisho kwa zambi zetu; wala si kwa zambi zetu tu, lakini kwa zambi za ulimwengu wote"*

(1 Yoane 2:2).

**2. Badilisho**

Kubadilisha ni kutumia kitu kimoja kwa pahali pa kitu kingine. Hata kama Mungu ni mapendo, Yeye ni Mwenye haki vilevile na amesema, "Nafsi inayofanya zambi itakufa" (Ezekieli 18:20). Hawezi kuona bule utaratibu ambao Yeye Mwenyewe aliusimamisha. Kwa mtu kupata wokovu, mambo saba yanahitajiwa:

(1) Sharti mtu mwingine afe kwa pahali pake. Kama sivyo, ni lazima kwa mwenye zambi kufa kwa zambi zake mwenyewe. Hakuna njia kwa yeye kupata wokovu.

(2) Sharti huyu atakayekufa kwa pahali pa mwenye zambi akubaliwe na Mungu.

(3) Sharti awe sawasawa na yule mwenye zambi. Au kusema, sharti awe mtu vilevile. Nyama hatoshi (Waebrania 10:4). Malaika hawezi kufa, kwa sababu ni roho. Ni lazima kwa yule atakayekufilia mtu kuwa mtu yeye mwenyewe.

(4) Sharti awe pasipo zambi. Kama akiwa na zambi, ingempasa kufa kwa zambi zake mwenyewe. Hataweza kufa badala ya mtu mwingine.

(5) Sharti akubali kufa. Si haki kwa Mungu kulazimisha mtu asiye na zambi kufa kwa mtu mwingine.

(6) Sharti awe na uzima kupita kadiri yote. Kama sivyo, mauti yake ingeweza kutosha kwa mtu mmoja tu. Sheria ya Mungu ndiyo hii, "Uzima kwa uzima" (Torati 19:21).

(7) Sharti awe Mungu Yeye Mwenyewe. Ni wazi ya kama Bwana Yesu Kristo tu aliye Mungu na mtu pamoja aliweza kutimiza maneno haya. Na vilevile kama mtu wa dunia akikufa kwa mtu mwingine, mshitaki, ndiye Shetani, angesema Mungu aliacha mtu kufanya kitu alichokataa kukifanya Yeye Mwenyewe! Lakini zaidi Mungu anataka mashukuru yetu na kuabudu kwetu kwa Yeye Mwenyewe (Kutoka 20:5).

Tunaona tena na tena ndani ya Biblia ya kwamba ni sharti kwa Mwingine kufa kwa ajili ya mtu. Zamani Mungu alipokea sadaka za nyama. Sadaka hizi hazikutosha kabisa kuondoa zambi, lakini zilikuwa mifano ya Kristo, kwani wakati nyama alipokufa, damu ilimwangika.

(1) Kwa mfano, Mungu alipokea mwana-kondoo ya Abeli, lakini alikataa sadaka ya Kaina kwa sababu haikuwa na damu (Mwanzo 4:4-5).

(2) Mungu alitayarisha kondoo ndume kufa kwa pahali pa Isaka (Mwanzo 22:13).

(3) Waisraeli walichinja elfu za nyama kama sadaka kwa Mungu kulipa kwa zambi zao (Walawi 1:4).

(4) Tunaona kweli ya badilisho wazi kabisa ndani ya Isaya 53:

"KWA makosa yetu" (sh.5);

"KWA maovu yetu" (sh.5);

"KWA sababu ya makosa ya watu wangu" (sh.8);

"zabihu KWA zambi" (sh.10).

(5) Yesu alisema juu ya mwili wake ambao aliutoa kwa ajili yetu na damu yake ambayo aliimwanga kwa ajili yetu (1 Wakorinto 11:24; Marko 14:24).

(6) Paulo alifundisha kweli hii vilevile. Ona Waroma 5:8 na Wagalatia 3:13.

(7) Hata Petro vilevile. Soma 1 Petro 3:18.

Ni ajabu kabisa! Kristo alikufilia wenye zambi. Alikufa kwa ajili yao, kwa faida yao. Alikufa kwa zambi, na alivumilia Yeye mwenyewe azabu iliyopasa wenye zambi kuipata. Kristo, Mwana wa Mungu, Mtu Mkamilifu, Yeye tu alitosha kabisa kwa kufa badala yetu.

**3. Upatanisho**

Katika Agano la Kale maana ya neno hili ni mara nyingi "Kufunika." Kabisa kabisa upatanisho haukuwa kufika siku Kristo alipokufa. Lakini kwa njia ya sadaka za nyama zambi "zilifunikwa" au kusamehewa kwa wakati. Mungu alikubali sadaka hizi za nyama kwa sababu alijua siku nyingine Kristo atakufa kwa zambi hizi (Waroma 3:25; Waebrania 9:15).

Tunapata maneno haya "upatanisho" na "kupatanisha" katika Agano Jipya vilevile. Kristo alitimiza kazi ya upatanisho kwa zambi zetu juu ya msalaba. Lakini upatanisho una maana nyingine vilevile. Ni kuondosha kuchukia na kuogopa na kugombana, na

kurudisha kwa upatano mzuri. Wakati mwenye zambi anapoamini Kristo, ni kazi ya Roho Mtakatifu kumpatanisha hivi na Mungu.

*"Wakati tulipokuwa adui, tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake"* (Waroma 5:10).

Hatusomi ndani ya Biblia juu ya Mungu akipatanishwa na watu. Anapenda watu tangu zamani. Ni SISI tunaohitaji kupatanishwa na Mungu. Halafu woga wetu na kuchukia kwetu kwa Mungu kunaondoshwa. Hii ndiyo kazi ya Roho Mtakatifu.

*"Mungu ambaye alitupatanisha sisi naye mwenyewe kwa Yesu Kristo"* (2 Wakorinto 5:18).

*"Akipatanisha ulimwengu naye mwenyewe"* (2 Wakorinto 5:19).

"*Mupatanishwe na Mungu"* (2 Wakorinto 5:20).

**4. Ukombozi**

Maana ya kukomboa ni kununua au kununua tena. Kwa mfano Mwisraeli akiwa mgonjwa au masikini, labda ilimpasa kuuza shamba lake kupata mali kwa mahitaji yake. Lakini kwa Sheria ya Musa, ndugu yake aliweza kulinunua tena wakati wo wote. Kwa njia hii aliweza kuchunga shamba hili kwa jamaa yao (Walawi 25:23-25). Soma habari za Ruta (Ruta 4:1-10) na Yeremia (Yeremia 32:6-12).

Katika Agano Jipya maneno mawili yalitumiwa kwa Kiyunani kwa kukomboa.

(1) Maana ya neno moja ni kununua. Mwana-kondoo (Kristo) ametununua kwa Mungu na damu yake mwenyewe (Ufunuo 5:9). Ametukomboa toka laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili yetu (Wagalatia 3:13).

(2) Maana ya neno la pili ni kufungua mtu au kumweka huru kwa njia ya kumlipia mali. Kristo alijitoa mwenyewe kwa sisi ili aweze kutukomboa toka uovu wote (Tito 2:14). Tumekombolewa toka mwenendo usiofaa, si kwa feza au zahabu, lakini kwa damu ya damani ya Kristo (1 Petro 1:18-19). Alitoa uzima wake uwe ukombozi wa watu wengi (Marko 10:45) na kutupatia ukombozi wa milele (Waebrania 9:12).

Mungu aliumba mtu, hivi mtu alikuwa mali yake. Lakini kwa sababu ya zambi mtu aliingia chini ya utawala wa mwingine, ndiye Shetani. Kristo alilipa ukombozi, alijitoa mwenyewe ili kununua mtu tena kwa Mungu. Hivi tunaona sisi si mali yetu wenyewe, lakini tumenunuliwa kwa bei, damu ya damani ya Bwana Yesu Kristo.

Ingetupasa kutukuza Mungu ndani ya miili yetu na ndani ya masemo na matendo yetu yote (1 Wakorinto 6:19-20).

## KAWAIDA YA WOKOVU

Mauti ya Kristo juu ya msalaba ni msingi kwa shauri la ajabu la Mungu kwa wokovu wa watu. Mauti hii ilikuwa sharti na ilitosha. Kuna maneno mane mengine ndani ya Biblia yanayoongeza tena mafundisho mengine juu ya kazi ya Mungu kwa kuokoa watu. Maneno haya ni:

MCHAGUO
KUWEKA TANGU ZAMANI
MWITO
KUWEKA KAMA WANA

Ndani ya sura hii tutawaza vilevile juu ya mambo mawili mtu anayohitaji kuwa nayo. Ni TOBA na IMANI.

### 1. Mchaguo

Tuliona mbele ya kama Mungu anajua maneno yote. Anajua mambo yatakayotokea wakati wa kuja. Basi Mungu anaongoza mambo yatakayotokea wakati wa kuja? Kusema Mungu anaJUA mambo yatakayotokea ni mbali na kusema anayaONGOZA.

Ndiyo, Mungu ni juu ya ulimwengu na mambo yote yaliyokwisha kutokea na yatakayotokea wakati wa kuja. Bila shaka mambo yote anayokusudi yatafanyikana. Lakini amempa kila mtu ruhusa kuchagua kitu anachotaka kukifanya, au uzuri, au ubaya.

Tunaona maneno ya kuchagua tena na tena ndani ya Biblia. Katika 1 Timoteo 5:21 tunasoma juu ya malaika wachagulifu. Israeli anaitwa mchaguliwa wa Mungu (Isaya 45:4), na kuna baki la Israeli “waliochaguliwa kwa neema ya Mungu” (Waroma 11:5). Kristo anaitwa mchaguliwa wa Mungu (Isaya 42:1; 1 Petro 2:6). Ndani ya Agano Jipya waamini wanaitwa “wachaguliwa wa Mungu” (Waroma 8:33; Wakolosayi 3:12).

Maana ya Mchaguo si kusema Mungu anachagua watu wengine wapate wokovu, halafu watu wote wanaobaki watapotea. Sivyo. Inapasa kila mtu kuchagua yeye mwenyewe wokovu wa Mungu. Kusudi la Mungu ni kutukuza Kristo. Kwa sababu hii Kristo ni Kichwa cha Kanisa linaloitwa vilevile mwili wake na bibi arusi yake. Kwa kutukuza Mwana wake, Mungu anapamba bibi arusi yake na kumpa baraka nyingi.

**2. Kuwekwa tangu zamani kwa Mungu**

Mungu alitangulia kutujua (1 Petro 1:2). Wale ambao Mungu aliwajua tangu zamani aliwaweka tangu zamani "wafananishwe na sura ya Mwana wake" (Waroma 8:29).

Mungu hakutuchagua tu, lakini alituchagua *zamani*. "Alitangulia kutuchagua ili tufanywe wana wake kwa njia ya Yesu Kristo kama ilivyopendeza mapenzi yake" na ".. sawasawa na kusudi lake" (Waefeso 1:5,11).

Ndiyo, Mungu alichagua watu na aliwaweka tangu zamani kwa Yeye Mwenyewe, lakini hata hivi Mungu atauliza watu juu ya maneno waliyofanya hapa duniani na kuwahukumu sawasawa na matendo yao. Sharti Habari Njema ihubiriwe kwa watu wote na kila mtu anayeamini ataokolewa. Lakini ni tamu kufikili ya kwamba Mungu alijua maneno yangu yote mbele, alinipenda hata wakati mimi nisipompenda Yeye, na alikusudi kunibariki sana ndani ya Kristo. Maneno haya yanaonyesha wazi ukubwa wake, na mapendo na uwezo wake.

**3. Mwito**

"Wale ambao aliwaweka tangu zamani, akawaita vilevile" (Waroma 8:30). Huu ndio mwito wa Habari Njema, njia ya Mungu kurudisha wenye zambi karibu naye. Kwa watu wengine Habari Njema inaonekana kuwa kitu kipumbavu, lakini wale ambao wanaiamini wanaona ndani yake mapendo ya Mungu waziwazi (1 Wakorinto 1:18). Hakuna mtu anayeweza kufika karibu na Kristo isipokuwa Mungu Baba anamvuta (Yoane 6:44). "Wote ambao Baba ananipa watakuja kwangu . . . naye anayekuja kwangu sitamtupa inje kabisa" (Yoane 6:37).

Mungu alichagua watu mbele ya kuwaita. Lakini hesabu ya wale wanaoitwa inapita mbali hesabu ya wale waliochaguliwa. "Wao wanaoitwa ni wengi, lakini wale wanaochaguliwa ni wachache" (Matayo 22:14).

**4. Kuwekwa kama wana**

Kazi nyingine ya Mungu ni kutuchagua kuwekwa kama wana wake (Waefeso 1:5). Tulifanyizwa wana wa Mungu dakika ile ile tulipozaliwa tena kwa njia ya kuamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wetu. Itaonekana wazi ya kama sisi ni kweli wana wakati Bwana Yesu Kristo atakapokuja na utukufu. Hivi tumepokea hata sasa roho ya kuwekwa kama wana, na tunangoja siku ile wakati mambo haya yatakapoonyeshwa wazi kwa dunia (Waroma 8:15,23). Neno hili litatokea wakati Bwana Yesu atakapokuja na miili yetu itakapokombolewa.

Kwa wenye zambi wanaoamini Kristo kuwekwa kama wana ni kazi ya Mungu Baba (Waefeso 1:5), ya Mungu Mwana (Wagalatia 4:5), na ya Roho Mtakatifu (Waroma 8:15).

Wokovu ni kazi ya Mungu tu peke yake. Mungu aliukusudi, aliutimiza na sasa anataka wenye zambi kuupokea bila kulipa. Upatanisho wa Kristo ni kwa dunia nzima (1 Yoane 2:2). Basi hivi watu wote wataokoka? Sivyo. Wale tu wataokoka wanaotubu zambi zao na walio na imani kupokea baraka za wokovu wa Mungu. Imani na toba si kazi njema mtu anazoweza kufanya. Hivi hakuna mtu anayeweza kujisifu mbele ya Mungu kwa sababu ya kazi zake njema.

**5. Toba**

Ndani ya Agano la Kale maana ya kutubu ni kuona huzuni kwa neno ulilofanya. Maana yake katika Agano Jipya ni kugeuza mafikili yako. Tunasoma mara moja moja juu ya kutubu kwa Mungu. Maana yake ndiyo kusema aligeuza mafikili yake juu ya watu. Wakati ninapotubu, ninageuza mafikili yangu:

(1) juu ya *zambi*. Ninafahamu sasa ya kuwa ni kuchukia na kuasi Mungu.

(2) juu ya *Mungu*. Ninafahamu sasa ya kwamba Yeye ni Rafiki.

(3) juu ya *Kristo*. Ninaona sasa ya kwamba Yeye anapita mbali watu wote kwa uzuri na ukubwa. (Wimbo wa Solomono 5:10,16).

Mungu anaagiza watu wote kutubu (Matendo 17:30).
Anawapa watu uwezo wa kutubu (Matendo 11:18).
Wema wake unatupeleka kwa toba (Waroma 2:4).
Bwana Yesu Kristo anaita watu kutubu (Luka 5:32).

Mtu akitubu anapata usamehe (Luka 24:47; Matendo 5:31). Halafu atataka kufanya kazi njema (Luka 3:8); na kubatizwa (Luka 3:3).

**6. Imani**

Imani ni kuamini masemo ya mtu mwingine. Kwa njia hii Mungu ametujulisha mapendo yake, na Mkristo anatangaza Habari Njema. Mtu anayeisikia na kuiamini ni mtu mwenye imani.

Neno hili "imani" linatumiwa vilevile kwa kweli zote za Mungu. Hivi katika Yuda 3 tunasoma, "Mushindane kwa imani waliyopewa watakatifu."

Tunasoma juu ya uaminifu wa Mungu vilevile (Waroma 3:3). Tunaweza kumwamini na kumtegemea kabisa na kujua atatimiza kwetu ahadi zake zote. Hivi tunaamini Habari Njema na ya kuwa Mungu ni mwaminifu. Tunajitia katika mkono wake. Neno hili ndilo imani.

Matendo ya mtu yanaonyesha kama akiwa na imani kweli au sivyo. Kukubali tu ya kwamba neno fulani ni kweli si namna ya imani Mungu anayotaka sisi kuwa nayo. Mashetani wanaamini kuna Mungu mmoja na wanatetemeka kwa woga, lakini neno hili haliwezi kuwaokoa. Kama imani ya mtu isipoonekana kwa njia ya matendo yanayopendeza Mungu, imani hii inakosa uzima, na mtu mwenyewe hana uzima wa milele hata kidogo (Yakobo 2:14-26).

Mchaguo, kuweka tangu zamani, mwito, na kuwekwa kama wana kunaonyesha ya kwamba Mungu ni juu ya mambo yote. Halafu karibu na watu Mungu anatafuta toba na imani.

## WOKOVU UNALETA NINI KWA MTU?

Mungu alilipa bei kubwa sana kwa wokovu wetu. Kwa njia ya kutubu na kuamini mtu anaweza kupokea wokovu huu. Halafu nini inatokea sasa? Wokovu huu ambao tunaupokea ni kitu gani? Maneno mane yanaonyesha mengine ya mambo ya ajabu tunayopata wakati tunapopokea wokovu wa Mungu.

*1. USAMEHE*

Zambi zetu zimesamehewa! Watu wengine wanasema hawana zambi. Wengine wanasema zambi zao si mbaya kama zambi za watu wengine. Ni vizuri zaidi kukiri zambi zetu mbele ya Mungu na kupokea usamehe wake.

Tunakuta neno hili "samehe" mara nyingi sana ndani ya Agano la Kale na Agano Jipya.

*"Utusamehe deni zetu"* (Matayo 6:12).

Zambi ni deni tuliyo nayo karibu na Mungu. Tuna deni kumpa Mungu maisha yetu, kumpenda na kumtii. Kwa sababu hatukumpa Mungu maneno haya, tumegeuka kama mtu yule katika Matayo 18:24 aliyekuwa na deni ya talanta elfu kumi karibu na mfalme, na aliyekosa mali kulipa deni yenyewe. Ndani ya mfano huu mfalme alihurumia mtu huyu na kumsamehe deni yake nzima. Mtu mwenyewe hakuhitaji kulipa hata nusu. Lakini Mungu kama MWAMUZI WA HAKI hawezi kusamehe zambi hivi. Anaweza kusamehe zambi kwa sababu moja tu: kwa sababu deni yenyewe imelipwa. Mkombozi, Bwana Yesu Kristo, aliilipa pia. Sasa Mungu anasame-

he zambi zetu, lakini zaidi ya ile, anazisahau vilevile. Mungu anaweza kujua mambo yote yatakayotokea na kuyasahau yale yanayokwisha kutokea!

*"Zambi zao sitazikumbuka tena"* (Waebrania 8:12).

Yule aliyesamehewa zambi zake akisikia habari hizi anaruka kwa furaha.

*"Mwana wangu, uwe na furaha; zambi zako zimesamehewa"* (Matayo 9:2).

*Heri waliosamehewa makosa yao"* (Waroma 4:7).

Mungu kama BABA anasamehe watoto wake kwa sababu nyingine. Si mapendo kwa Baba kuniacha kuendelea kwa zambi. Kama nikianguka kwa zambi, furaha yangu inapotea. Baba yangu atanisamehe KAMA nikikiri zambi zangu.

*"Tukikiri zambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote"* (1 Yoane 1:9).

Kwa sababu niliamini Kristo, mimi ni sasa mtoto wa Mungu, ndani ya jamaa yake. Mkristo mwingine, ndugu yangu kwa Kristo, akinikosea, ninamsamehe kwa sababu zambi zangu mwenyewe zimesamehewa (Waefeso 4:32; Wakolosayi 3:13), si kwa sababu mwingine alilipa kwa zambi hii namna Kristo alivyolipa kwa zambi zetu. Nikitaka Baba kunisamehe, sharti nisamehe ndugu zangu vilevile (Matayo 6:14-15; 18:32-35).

*2. KUHESABIWA HAKI*

Ndani ya Agano la Kale tunapata mafundisho juu ya usamehe wa zambi, lakini mafundisho juu ya kuhesabiwa haki yanapatikana katika Agano Jipya tu, zaidi ndani ya barua za Paulo. Usamehe na kuhesabiwa haki ni mbalimbali kwa njia gani?

Wakati tunaposamehewa, deni tuliyokuwa nayo kwa sababu ya zambi zetu imeondoshwa. Wakati tunapohesabiwa haki tunapata cheo kipya mbele ya Mungu. Ndani ya Agano la Kale labda mtu alihitaji kusamehewa tena na tena, lakini ndani ya Agano Jipya mtu anahesabiwa haki mara moja tu. Hatahitaji kuhesabiwa haki tena kamwe.

Basi maana ya kuhesabiwa haki ni nini?

(1) Maana yake HAIKO kuwa haki. Mtu si mwenye haki, hata kama anaweza kuhesabiwa haki. *"Hakuna mwenye haki, hata mmoja"* (Waroma 3:10).

(2) Maana yake HAIKO kufanyiza mtu kuwa mwenye haki. Wakati Mungu anapohesabu mtu haki, hamgeuzi kuwa mwenye haki.

(3) Wakati mtu anapohesabiwa haki, Mungu anasema yeye ni mwenye haki sasa kwa sababu yeye ni ndani ya Kristo. Mtu aliye ndani ya Kristo si chini ya hukumu ya zambi tena na hahitaji kulipa kwa zambi zake (2 Wakorinto 5:21). Ni kwa sababu hakufanya zambi? Sivyo, lakini ni kwa sababu Bwana Yesu Kristo alibeba azabu kwa zambi zake. Hivi sheria ya Mungu haiwezi kumhukumu tena.

*"Ni nani atakayeshitaki wachaguliwa wa Mungu?*
*Mungu ndiye ambaye anawahesabia haki"* (Waroma 8:33).

Katika Waroma tunaona watu wanahesabiwa haki

(1) kwa neema (3:24);

(2) kwa haki (5:18-19), ndiyo kutii kwa Kristo juu ya msalaba;

(3) kwa damu (5:9), ambayo Bwana Yesu Kristo aliimwanga kwa Kalvari;

(4) kwa ufufuko (4:25), ufufuko wa Kristo uliohakikisha ya kwamba Mungu alikubali sadaka ya mauti ya Kristo msalabani;

(5) kwa imani (5:1), inayoonyesha ya kuwa mtu amepokea sadaka ya Kristo kwa ajili yake.

Tunasoma watu wanahesabiwa haki kwa njia ya matendo vilevile (Yakobo 2:21-25). Maana yake hii: Kwa njia ya matendo yake mema mtu anaonyeshea watu wengine ya kwamba amehesabiwa haki. Wale waliohesabiwa haki wana salama mioyoni mwao (Waroma 5:1).

*3. UPATANISHO*

Vizuri msomaji asome tena mafundisho juu ya upatanisho kwa ukurasa 52.

Mungu ni mapendo, naye hageuki kamwe. Hawezi kubadilika. Amependa watu tangu zamani, lakini kwa sababu watu hawakujua neno hili, waliogopa Mungu na kumchukia. Lakini Mungu alifunua na kuhakikisha mapendo yake kwa watu kwa Kalvari. Wakati mtu anapoamini kweli ya kwamba Mungu anampenda, hamwogopi wala kumchukia tena. Anapenda Mungu sasa. Amepatanishwa naye. Hakuna neno tamu kuliko kuwa na upatano mzuri na Mungu.

*"Wakati tulipokuwa adui, tulipatanishwa na Mungu kwa kufa kwa Mwana wake"* (Waroma 5:10).

*"Nanyi muliotengwa mbali zamani na mulikuwa adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha nyinyi sasa"* (Wakolosayi 1:21-22).

*4. KUZALIWA TENA*

Tunaweza kufikili juu ya mauti kama kutengwa kwa mwili na roho. Vivyo hivyo kufa kwa roho ni kwa mtu kutengwa na Mungu. Ni tunda la zambi.

*"Wafu kwa sababu ya makosa yenu na zambi zenu"* (Waefeso 2:1).

Kila mtu duniani anazaliwa na uzima wa Adamu ndani yake. Uzima huu ni mzuri kwa kuishi hapa duniani, Iakini hautoshi kwa mbingu.

*"Ila mtu azaliwe mara ya pili hawezi kuona ufalme wa Mungu"* (Yoane 3:3).

Biblia inatuonyeshea namna gani tunaweza kuzaliwa tena. Tunazaliwa tena kwa Roho ya Mungu na kwa Neno la Mungu (Yoane 3:5; 1 Petro 1:23). Mtu hawezi kuzaliwa mwana wa Mungu kwa njia ya:

(1) damu (sadaka ya nyama, au kwa sababu mama na baba yake ni Wakristo);

(2) mapenzi ya mwili (kwa sababu yeye mwenyewe anakusudi kuzaliwa tena);

(3) mapenzi ya mtu (kwa kusaidia au maombi ya mtu mwingine).

Wale wanaozaliwa wana wa Mungu ndio wale wanaopokea Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao kwa njia ya kuamini jina lake (Yoane 1:12-13).

Wakati ninapozaliwa tena, ninageuka kiumbe kipya ndani ya Kristo. Maneno ya zamani yamepita na maneno yote yamekuwa mapya (2 Wakorinto 5:17). Ninavaa mtu mpya (Wakolosayi 3:10). Halafu ninaweza kutembea katika upya wa uzima.

Kama mwana wa Mungu mimi ni mriti vilevile, mriti pamoja na Mwana wa Mungu (Waroma 8:17; Wagalatia 4:7). Baba atanihamakia na kuniazibu kama nikimwasi. Hafanyi hivi kwa watu wote, lakini kwa wana wake wapendwa tu (Waebrania 12:6).

## MATUNDA YA WOKOVU

Watu waliookolewa ndio wale waliopokea wokovu. Neno hili wokovu linapasha juu ya mambo mengi ya ajabu ambayo Mungu anatayarishia wale wanaopokea Kristo. Mengine ya mambo haya yamepita na hayataweza kugeuzwa tena kamwe. Mengine yana-endelea siku kwa siku.

*"Mukipokea . . . wokovu wa nafsi zenu" (*1 Petro 1:9).

Mengine yatatimia wakati wa kuja.

*"Wokovu ulio tayari kufunuliwa kwa wakati wa mwisho"* (1 Petro 1:5).

Ndani ya sura hii na ile inayofuata tutazungumuza juu ya baraka tunazopata sasa kwa njia ya wokovu.

Maana ya neno hili "takasa" ni kuweka mbali kwa Mungu. Mungu ni mtakatifu, hivi kutakasa ni kufanyiza mtu kuwa mtakatifu. Waamini wote ni watakatifu (Waroma 1:7). Wametakaswa, au kuwekwa mbali kwa Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Lakini utakaso ni neno linaloendelea kila siku vilevile.

Utakaso si neno la wakati wa sasa tu. Ni neno lililokwisha kufanywa (1 Wakorinto 6:11), na litaendelea kufika siku Kristo atakapotukamilisha (Waefeso 5:26-27).

Tuwaze sasa juu ya mambo makubwa matatu: KUSHINDA, KUZAA MATUNDA, na KUJUA KABISA.

### 1. Kushinda

Sehemu ya wokovu INAYOPITA iliniokoa toka AZABU ya zambi.

Sehemu ya wokovu kwa WAKATI WA SASA inaniokoa toka UWEZO wa zambi.

Sehemu ya wokovu kwa WAKATI WA KUJA itaniokoa toka UKARIBU wa zambi.

Wokovu wetu wakati wa sasa unatuwezesha kushinda adui zetu. Mwamini ana adui tatu: dunia, mwili, na Shetani (Waefeso 2:2-3). Kwa njia hizi tatu zote anasukumwa kufanya zambi.

**Mwili** huu si mwili wa nyama na mifupa na damu tu. Neno hili linatumiwa vilevile ndani ya Biblia kwa kutaka kwa mtu kufanya zambi (Wagalatia 5:17). Hata wakati mtu alipozaliwa tena, mwili huu ungali, na utakuwa pamoja naye kufika siku ya kuondoka kwake duniani. Unamsukuma kufanya zambi kwa njia ya desturi mbaya alizokuwa nazo mbele ya kuokolewa (Waroma 7:5), na kwa njia ya tamaa (1 Petro 2:11).

**Dunia** ni adui ya mwamini vilevile. Dunia ndiyo watu waovu

ambao wanamzunguka kila siku. Watu wote, lakini zaidi vijana, wanafikili sharti waige rafiki zao. Hivi dunia inatujaribu kwa njia ya kutusukuma kuiga mambo mabaya (1 Petro 4:4).

Watu wengi wanaofanya zambi wanatoa uzuru kwa njia ya kusema ni Shetani ambaye aliwajaribu. Basi Shetani hawezi kuwa kila pahali duniani kwa saa moja, na kazi yake kubwa si kuangusha Wakristo. Ukitaka kujua sababu ya zaidi ya zambi zako, angalia ndani ya roho yako tu!

Labda kazi kubwa zaidi ya Shetani ni kwa njia ya dini za uwongo (2 Wakorinto 11:13-15). Anatawala juu ya majeshi ya madaimoni wanaofanya mapenzi yake. Kusudi lake kubwa ni kuamsha shaka na mawazo mabaya ndani ya nia za watu, kama tulivyoona katika Mwanzo 3:1-5.

Basi mwamini aliye zaifu anaweza namna gani kushinda adui hawa wenye uwezo mkubwa? Biblia inatuonyeshea njia:

(1) Tunakatazwa kupenda **dunia**, lakini tunaagizwa kupenda Baba Mungu (1 Yoane 2:15; Wakolosayi 3:2).

*"Dunia hii imesulibiwa kwangu, na mimi kwa dunia"* (Wagalatia 6:14).

(2) Wale walio watu wa Kristo wamesulibisha **mwili** (Wagalatia 5:24), hivi haifai kwao kuweka roho juu ya mahitaji yake ya kufanya zambi (Waroma 13:14). Tukikwenda kwa Roho, hatutatimiza tamaa za mwili (Wagalatia 5:16).

(3) "Mushindane na **Shetani**, naye atawakimbia ninyi" (Yakobo 4:7). Kristo aliona Shetani akianguka toka mbingu kama umeme (Luka 10:18). Bila shaka Shetani ataharibiwa (Waebrania 2:14).

**2. Kuzaa matunda**

Mtu anayeshinda dunia, mwili, na Shetani ndani ya maisha yake ya kila siku ni Mkristo kweli. Neno lingine linaloonyesha ya kwamba amezaliwa tena ni matunda atakayozaa. Basi matunda haya ni nini?

(1) Matendo mema yanaitwa matunda (Matayo 3:8). Yanahakikisha ya kuwa mtu alitubu na sasa yeye ni mtoto wa Mungu kweli. Kwa njia ya matunda mtu anayozaa unaweza kujua kama yeye ni nabii wa Mungu au nabii wa uwongo (Matayo 7:16).

(2) Mtu anayetembea kwa Roho anazaa matunda ya Roho tunayoona ndani ya Wagalatia 5:22-23: mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, ujizuiza.

(3) Paulo alisema Habari Njema ilizaa matunda ndani ya dunia nzima. Matunda haya yalikuwa watu waliookolewa wakati waliposikia Habari Njema. Alitaraji atakuwa na matunda kwa Roma vilevile kama alivyokuwa nayo pahali pengine. Mtu akiwa na hamu kupasha watu wengine juu ya Kristo na njia ya wokovu, neno hili linaonyesha ya kwamba ameokoka. Ni neno zuri sana kuleta mtu mwingine karibu na Bwana Yesu Kristo. Lakini Biblia inafundisha ya kuwa KUISHI kwa Mungu kila dakika, kila siku, kila mwaka, ni neno hata kubwa kuliko kushuhudia Kristo.

Unaweza kuzaa matunda kwa Mungu namna gani? Yesu alisema, *"Mwenye kukaa ndani yangu, na mimi ndani yake, huyu anazaa sana . . . Kwa hivi Baba yangu anatukuzwa, muzae matunda mengi"* (Yoane 15:5,8).

Tawi (Mkristo) akizaa matunda, Baba (Mungu) analisafisha ili liweze kuzaa matunda mengi zaidi. Kama lisipozaa matunda, linaondoshwa ndani ya mzabibu (Mwana Yesu Kristo). Maana yake ndiyo hii: kama mwamini asipozaa matunda, labda Baba atampeleka mbinguni ili mwamini huyu asimpatishe haya hapa duniani.

**3. Kujua kabisa**

Tunda moja la Roho ni salama (Wagalatia 5:22). Lakini namna gani mwamini ataweza kuwa na salama moyoni mwake kama akiogopa labda atapoteza wokovu wake tena? Mungu hataki tusumbushwe na woga kama huu. Alitupa sisi wokovu wa **milele.** Halafu anataka tujue ya kama tumepata wokovu kweli na kuwa na salama moyoni. Tunda moja zuri sana la wokovu ni hili: tunaweza kujua bila shaka ya kwamba tumeokoka na hatutaweza kupotea tena kamwe.

Biblia inafundisha ya kwamba msingi wa wokovu wetu ni kazi ambayo Bwana Yesu Kristo aliitimiza wakati alipokufa juu ya msalaba kwa zambi zetu. Kama ingalinipasa kutegemea kazi zangu njema kuniokoa, siwezi kujua kamwe kama nimeokoka. Lakini kuwa na shaka juu ya wokovu wetu ni kutokuamini, na kutokuamini ni zambi.

> *"Ninawaandikia ninyi wenye kuamini jina la Mwana wa Mungu, maneno haya, ili MUJUE ya kuwa MUNA uzima wa milele"* (1 Yoane 5:13).

Kwa sababu ya kazi ya Kristo hatuwezi kupotea tena kamwe. Wakati tunaposoma maneno haya ndani ya Biblia, Neno la Mungu, na kuyaamini, tunapokea salama rohoni kwani tunajua kabisa ya kwamba tumeokoka kwa milele.

Mkristo aliye na shaka juu ya neno hili anazidi kusumbuka na kujaribu kutenda matendo mema ili wokovu wake usimpotee. Lakini anafanya kazi njema hizi kwa kujisaidia mwenyewe, asipotee, si kwa kupendeza Mungu. Kazi hizi haziwezi kufurahisha Mungu. Lakini kazi tunazofanya kwa utukufu wake tu zinamfurahisha zaidi.

Biblia inafundisha ya kwamba mwamini wa kweli hawezi kupotea tena kamwe. Watu wengine hawaamini neno hili. au wanafikili maana yake ni kusema Mkristo anaweza kutembea sawasawa roho yake inavyotaka. Lakini tumeona mbele ya kuwa Mungu Baba ataazibu watoto wake kama wakimwasi.

Watu hawa wanafikili wanaweza kuonyesha wazi ndani ya Biblia ya kwamba mwamini anaweza kupotea tena. Kwa kufanya hivi wanatumia mashairi haya:

(1) “Mwenye kuvumilia hata mwisho ataokolewa” (Matayo 24:13). Lakini shairi hili linafundisha juu ya Wayuda kwa wakati wa Mateso Makubwa, si juu ya Mkristo anayejaribiwa kufanya zambi.

(2) “Timizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka” (Wafilipi 2:12). Lakini shairi hili halisemi “Tumikeni KUPATA wokovu.” Shairi 13 linaonyesha wazi ya kwamba ni Mungu anayetenda kazi ndani yetu.

(3) “Na kisha walianguka, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu” (Waebrania 6:4-6). Mashairi haya yanafundisha juu ya Wayuda walioacha dini yao. Kama kweli yangalifundisha juu ya Mkristo aliyerudi nyuma na asiyefuata Bwana tena, yangalisema Mkristo huyu hawezi kurudishwa karibu na Bwana kamwe!

(4) “Hakuna mtu anayeweza kuwanyanganya toka mkono wangu” (Yoane 10:28). Lakini nini itatokea kama nikijiondosha mwenyewe toka mkono wa Kristo kwa njia ya kufanya zambi? Hata nikifanya zambi siwezi kupotea, kwani ndani ya shairi hili Yesu anasema, “Hawatapotea hata milele.”

Kuna mashairi mengi ndani ya Agano Jipya yanayofundisha ya kama mwamini wa kweli anaweza kujua hakika yeye si katika hatari ya kupotea tena.

> *“Naye anayekuja kwangu sitamtupa inje kabisa”* (Yoane 6:37).
>
> *“Kila mtu mwenye uzima na kuniamini mimi hatakufa hata milele”* (Yoane 11:26).

*"Ndani yake mumekwisha kuamini vilevile na kutiwa muhuri wa Roho Mtakatifu ya ahadi"* (Waefeso 1:13; 4:30).

*"Utajiri wote wa kufahamu kwa hakika"* (Wakolosayi 2:2).

*"Ninamjua yeye ambaye nilimwamini, na ninajua kabisa . . ."* (2 Timoteo 1:12).

*"Anaweza kuokoa kabisa wao wanaokuja kwake Mungu"* (Waebrania 7:25).

*"Wapenzi, sasa tuko wana wa Mungu"* (1 Yoane 3:2).

Ukisema sharti utumike kazi upate wokovu au uchunge wokovu wako, unasema kazi Kristo aliyofanya msalabani haitoshi. Kusema hivi ni vibaya sana, kwani kunapatisha jina la Kristo haya kabisa. Mwana wa Mungu ni Mwenye uwezo kutuokoa (Isaya 63:1), na kutulinda (Yuda 24).

## BARAKA ZA WOKOVU

Tumepatanishwa na Mungu kwa damu ya Yesu. Hatuhitaji kuogopa tena, lakini tunapata ruhusa na uhodari kufika mbele ya Mungu. Tuna Kuhani Mkubwa vilevile, Bwana wetu Yesu Kristo. Hivi tunaweza kukaribia "kwa moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani" (Waebrania 10:19-22). Baraka kubwa mbili nyingine ambazo Mkristo anazipokea ni ruhusa ya kuomba na kuabudu Bwana.

### 1. Maombi

Ruhusa ya kuomba ni kitu kitamu sana tunachopata kwa njia ya wokovu. Ni kitu ambacho kinatusaidia kabisa ndani ya maisha yetu kwa Kristo siku kwa siku. Biblia inatufundisha nini juu yake? Tuone sheria kubwa mbili za maombi:

(1) Ya kwanza inasimama juu ya mapendo na uwezo wa Mungu. Ndiyo hii: **Mungu atakupa kila kitu unachoomba kwa jina la Yesu**. Waza juu ya mashairi haya:

*"Kila mtu anayeomba anapokea"* (Matayo 7:7-8).

*"Kama mukiomba neno gani kwa jina langu, nitalifanya"* (Yoane 14:14).

*"Kila neno munaloomba Baba kwa jina langu, atawapa nini"* (Yoane 16:23).

(2) Mashairi haya na mengine mengi yanatuonyeshea sheria ya kwanza ya maombi. Lakini sheria ya pili inaweka mpaka kwa she-

ria ya kwanza. Inasimama juu ya akili na utakatifu wa Mungu. Sharti mapendo na uwezo wake zitumike pamoja na akili na utakatifu wake. Sheria ya pili inasema ya kuwa **Mungu atawapa watu wake mambo yaliyo kwa baraka yao tu.**

*"Baba yenu aliye mbinguni atawapa wale ambao wanamwomba vitu vizuri," si mawe au nyoka* (Matayo 7:9-11).

*"Mukiomba . . . nitalifanya, Baba atukuzwe ndani ya Mwana"* (Yoane 14:13).

Kama neno ninalotaka kuomba lisipoweza kutukuza Baba, haifai kwangu kuliomba. Lakini kama nikiliomba hata hivi, Mwana wa Mungu hatanipa neno lenyewe. Au labda ninaomba Mungu kwa neno ninalofikili litanifurahisha. Lakini kwa pahali pa kunipa neno nililoomba, Mungu ananipa neno lingine ambalo litanifurahisha zaidi wakati wa sasa na hata milele.

*"Furaha yenu itimizwe"* (Yoane 16:24).

Neno ambalo linatufazaisha zaidi kwa maneno ya maombi ndilo hili: Nikiomba Mungu kunipa kitu ninachotaka, Mungu atanipa kitu chenyewe? Ndiyo, Mungu atakupa kitu chenyewe kama kikipatana na mapenzi yake. Kama sivyo, atakataa, lakini atakupa kitu kizuri zaidi. Sheria mbili za maombi tulizotaja sasa tu zinaonyesha kwa sababu gani anafanya hivi.

Mungu alijibu maombi ya watu wengi kwa wakati wa Agano la Kale na Agano Jipya. Anafanya hivi hata leo. Mara nyingine alijibu maombi yao kwa njia ya kusema, "Hapana." Hata leo anafanya vile. Kwa mfano:

Musa aliomba ruhusa kuweza kuingiza Waisraeli katika inchi ya Kanana, lakini Mungu alikataa (Torati 3:23-26).

Daudi aliomba mtoto wake aweze kuishi, lakini Mungu alikataa (2 Samweli 12:16,19).

Paulo aliomba mateso aliyokuwa nayo katika mwili wake yaweze kumwondokea, lakini Mungu alikataa (2 Wakorinto 12:8-9).

Mara nyingine Mungu alingoja kwanza kwa wakati mbele ya kujibu maombi, na kwa njia hii alipata utukufu mkubwa zaidi. Kwa mfano: Mkubwa wa sunagogi aliomba binti yake aponyeshwe. Mtoto alikufa, lakini Kristo alimfufua tena toka wafu (Marko 5:23, 35-42).

Maria na Marata walipasha Bwana Yesu habari za ugonjwa wa ndugu yao. Wakati Yesu alipofika kwao, Lazaro alikuwa amekufa, lakini Bwana alimfufua tena (Yoane 11:3,14,44).

Kuna uwezo mkubwa ndani ya maombi. Hata wakati Bwana Yesu alipoomba, aliongeza maneno haya, "si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka" (Marko 14:36).

Mara nyingine Mungu anajibu maombi yasiyopatana na mapenzi yake. Kwa mfano:

Waisraeli walinungunika juu ya chakula ambacho Mungu aliwapa na waliomba kupewa nyama. Mungu aliwapa nyama, lakini aliwaazibu vilevile (Zaburi 106:15).

Wagerase waliomba Yesu kuondoka kwao — naye alikwenda zake! Ona Marko 5:1-17.

Maombi ni baraka kubwa, na vilevile ni kazi kubwa ambayo Mungu anatupa sisi. Kila mara tunapopiga magoti kwa kuomba, ni kama Kristo anatuuliza:

*"Munataka niwafanyie ninyi nini?"* (Matayo 20:32).

*"Munaamini ya kama ninaweza kufanya neno hili?"* (Matayo 9:28).

Tunaweza kujumlisha sheria mbili za maombi na maneno haya ya Yakobo:

1. *"Hamuna kitu kwa sababu hamwombi"* (Yakobo 4:2).
2. *"Munaomba wala hamupati kwa sababu munaomba vibaya"* (Yakobo 4:3).

**2. Kuabudu**

Kwa sababu gani Mungu alitupa sisi ahadi hizi juu ya maombi? Ili tuweze kushiriki ndani ya kazi ya kutawala ulimwengu huu? Sivyo, lakini ili tuweze kumsifu Yeye wakati anapojibu maombi yetu. Kushukuru Mungu ni neno kubwa kuliko hata maombi. Maneno haya yanatufikisha kwa baraka kubwa nyingine, ndiyo KUABUDU. Ni kusudi la Mungu kwa sisi kuwa "Sifa ya utukufu wake" (Waefeso 1:12).

Kuabudu ni kumwambia Mungu ya kwamba tunampenda sana na tunafikili Yeye ni mzuri kupita wote. Ni hata kukubwa kupita kushukuru.

Bwana Yesu alitufundisha nini juu ya kuabudu? Mashairi yenye mafundisho makubwa zaidi juu ya kuabudu ni katika Yoane 4. Sura hii inatufundisha ya kwamba:

(1) Hatuhitaji kwendea pahali fulani au nyumba fulani kuweza kuabudu Mungu (mash.21-23).

(2) Sharti tuabudu Mungu na roho zetu kwa sababu Mungu ni Roho (sh.24; Wafilipi 3:3).

(3) Sharti kuabudu kwetu kupatane na kweli ya Mungu (sh.24). Watu wengine wanafikili wanaweza kuabudu Mungu wakiiga desturi za watu. Lakini sivyo. Kuabudu namna hii ni bule (Matayo 15:8-9).

(4) Kuabudu kwetu ni neno kubwa kwa Mungu Baba. Anawatafuta wale ambao wanamwabudu katika roho na kweli (sh.23).

(5) Wale tu wanaojua Mungu ni Baba yao wanaweza kumwabudu. Neno hili linawezekana kwa njia ya Kristo tu (Yoane 14:6).

Wakati watakatifu (waamini wa kweli) wanapokutana pamoja kukumbuka Bwana, wanaweza kuabudu Mungu. Lakini mwamini anaweza kunyanyua roho yake kwa Mungu na kumwabudu wakati wo wote na pahali po pote.

Zambi moja ya wapagano ndiyo hii: Hawashukuru Mungu (Waroma 1:21). Lakini wema wake kwa watu wote unaonekana wazi (Matendo 14:17; 17:25).

KUSIFU Mungu ni neno kubwa kuliko kumshukuru tu. Wakati ninaposifu Mungu ninampasha ya kwamba Yeye ni kweli Mungu wa ajabu. Ninaweza kumsifu kwa kazi zake, au kwa namna alivyo Yeye Mwenyewe. Sifa kwa namna Mungu alivyo ina faida kuliko sifa kwa kazi zake, kwani Mungu ni mkubwa kupita zawadi zake ambazo anawapa watu.

KUABUDU kunafanana na kusifu Mungu kwa namna alivyo Yeye Mwenyewe. Ni hali ya roho. Tunaweza kuabudu Mungu bila kusema neno au kwendea pahali fulani au kupiga magoti au neno lo lote lingine. Tunahitaji maneno mawili tu, ndiyo roho inayojaa na mapendo kwa Mungu, na nia inayowaza juu ya maajabu yake yote.

Kwa njia nyingine USHIRIKA na Mungu ni hata mkubwa kuliko sifa na kuabudu. Ni kushiriki na Mungu ndani ya mawazo yake na kutaka kwake. Mungu anaheshimu Kristo sana? Ninaweza kushiriki ndani ya mawazo haya na kumheshimu vilevile. Kristo anapenda Kanisa? Ninaweza kushiriki ndani ya mapendo haya.

Tusikose kamwe kuwa na roho ya asante. Wakoma tisa walisafishwa, lakini hawakurudi kumpa Bwana asante, naye alihuzunishwa (Luka 17:17). Lakini wakati tunapojua Mungu kweli kweli kuna kazi nyingine kwa roho zetu zinazopita kuleta asante tu, ndizo hizi: **Sifa, kuabudu na ushirika**. Hakuna neno lililo zuri kupita kwa mtu yule anayetembea karibu sana na Mungu.

# KANISA

Kanisa gani ndilo kanisa la kweli? Watu wengi wanauliza kwa sababu gani kuna makanisa namna mbalimbali duniani leo. Tuone basi mafundisho ya Biblia juu ya neno hili.

Kwa wakati wa sasa watu wana mawazo namna namna juu ya kanisa. Lakini wenye elimu wanapatana ndani ya maneno wana-yoyasema juu ya namna ya kanisa kwa wakati wa mwanzo wake, wakati Agano Jipya lilipoandikwa sasa tu, muda mfupi nyuma ya kufa na ufufuko wa Kristo. Hivi ingekuwa neno jepesi kuwa na kanisa leo lililo sawasawa na kanisa la wakati wa mwanzo. Lakini Wakristo wengi wanafikili hatuhitaji kuiga mfano huu wa kanisa ambao tunaupata ndani ya Agano Jipya. Wanasema utaratibu wa kanisa lile la mwanzo hauwezi kutosha vizuri wakati wa sasa. Wanaanguka ndani ya mawazo haya.

## KANISA NI NINI?

Maana ya neno linalotafsiriwa kanisa ndani ya Agano Jipya ni watu wanaokwisha kuitwa kutoka katikati ya watu wengine kuwa kundi moja. Linatumiwa kwa waamini wote wa kweli toka siku ya Pentekote, kufika siku Kristo atakapokuja tena. Nyumba pahali Wakristo wanapokusanyika kuabudu Mungu haikuitwa kanisa ndani ya Agano Jipya.

Kanisa linaitwa MWILI wa Kristo (Waefeso 1:22-23). Kristo ni Kichwa cha Mwili huu, naye ni mbinguni. Wakristo ni kama viungo mbalimbali vya mwili (1 Wakorinto 12:12-13). Kila mmoja ana kazi kubwa ambayo inampasa kufanya.

Kanisa ni kama JENGO kwa Waefeso 2:20-22. Kristo ni Jiwe kubwa la pembeni la jengo hili (1 Petro 2:7). Hivi Kanisa ni kama hekalu, pahali Mungu anapoweza kukaa. Roho ya Mungu anakaa ndani ya waamini wote.

Kanisa ni vilevile kama BIBI ARUSI ya Kristo (Waefeso 5:25-27). Neno hili linatukumbusha mapendo makubwa Kristo aliyo nayo kwa Kanisa. Anatunza Kanisa lake hapa duniani. Siku nyingine atakuja kulipeleka Kwake mbinguni kwa milele.

Neno hili kanisa linatumiwa vilevile kwa waamini wanaokaa katika kijiji kimoja (1 Wakorinto 1:2). Labda wao ni wawili au

watatu tu (Matayo 18:20). Neno kubwa ndilo hili: Kristo ni pamoja nao.

Ni neno kubwa vilevile kwa kila kanisa kwa pahali fulani (ndio waamini wa pahali pale) kuwa mfano mzuri wa Kanisa zima, ndilo Mwili wa Kristo. Kristo ni Kichwa cha Kanisa? Halafu inapasa waamini ndani ya kanisa la pahali fulani kumpa pahali pa kwanza katikati yao. Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Kanisa? Halafu sharti waamini wa makanisa wanaokusanyika kwa miji na vijiji mbalimbali waongozwe na Roho Mtakatifu. Wakristo wote ni viungo vya mwili wa Kristo, hivi inapasa kuwapokea ndani ya kanisa linalokutana kwa pahali fulani. Lakini kama Wakristo hawa wakifundisha maneno yasiyopatikana ndani ya Biblia au kama wakitembea kwa zambi, haifai watu wa kanisa kuwapokea. Roho Mtakatifu anahuzunishwa wakati waamini ndani ya kanisa wanapotembea kwa zambi.

## KAZI KUBWA ZA KANISA LA PAHALI FULANI NI NINI?

Tumeona ya kwamba Mungu anawatafuta wale ambao watamwabudu katika roho na kweli. Ndiyo, unaweza kuabudu Mungu peke yako. Unaweza kuomba peke yako vilevile, na kuhubiri peke yako, au kufundisha mtu mwingine bila kuwa na Wakristo wengine pamoja nawe. Kwa sababu gani basi inatupasa kukusanyika pamoja kama kanisa?

Ni kutaka kwa Mungu kwa sisi kutumika na kuabudu pamoja.

> *"Mmoja atafukuza elfu, na wawili kukimbiza elfu kumi"* (Torati 32:30).
>
> *"Tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine"* (Waebrania 10:25).

Ndani ya kitabu cha Matendo tunasoma habari za Kanisa kwa wakati wa mwanzo wake. Tunaona pale ya kuwa Wakristo walikutana pamoja wakati na wakati. Walidumu "katika mafundisho ya mitume, na katika ushirika, na katika kuvunja mkate na kuomba" (Matendo 2:42). Haya ndiyo maneno Wakristo wa wakati wa mwanzo waliyofanya zaidi.

(1) **Mafundisho**. Watu wa kanisa walikusanyika kusikia Neno la Mungu. Maandiko Matakatifu yanaweza kutupatia akili kupata wokovu (2 Timoteo 3:15). Mungu anatumika na Neno lake kwa kututakasa (Yoane 17:17). Biblia inaweza kutujenga vilevile na kutupatisha nguvu katika imani (Matendo 20:32).

Sura 12 ya 1 Wakorinto inatufundisha ya kuwa inapasa viungo vyote vya mwili wa Kristo kusaidiana. Ndani ya 1 Wakorinto 14 tunaona namna gani Wakristo waliongoza makusanyiko yao. Labda watu wawili au zaidi walifundisha Neno la Mungu (sh.26), lakini wote waliosema maneno waliongozwa na Roho Mtakatifu, hivi mambo yote yalifanywa kwa utaratibu.

(2) **Kuvunja mkate**. Mbele ya kufa kwake, Bwana Yesu aliomba wanafunzi wake kuvunja mkate na kunywa kikombe kwa kumkumbuka Yeye kufika siku atakapokuja tena.

Ni neno kubwa sana kwa sisi kukumbuka Bwana. Hatutaki kuwa watu wanaokosa kuwa na roho ya asante, watu wa kusahau mbio mbio. Vitu hivi Bwana alivyochagua vinaweza kutukumbusha Bwana wetu na kazi yake msalabani vizuri kuliko vitu vyo vyote vingine. Mkate ni mfano wa mwili wake ambao aliutoa kwa sisi. Kikombe ni mfano wa damu yake iliyomwangika kwa ajili yetu. Mauti yake inahakikisha kupita mambo yote mengine mapendo yake makubwa kwa sisi.

Petro anasema waamini wote ni makuhani (1 Petro 2:5,9). Tuna ruhusa kufika mbele ya Mungu (Waebrania 10:19-22), na tunaweza kutoa sadaka vilevile:

Miili yetu (Waroma 12:1)
Sifa yetu (Waebrania 13:15)
Zawadi zetu (Waebrania 13:16)

Saa nzuri zaidi kwa Wakristo kuabudu pamoja ni wakati wanapokusanyika kuvunja mkate na kunywa kikombe kukumbuka kufa kwa Bwana yao. Inatupasa kufanya hivi mara ngapi? Hakuna agizo juu ya neno hili ndani ya Agano Jipya, lakini ni kama Wakristo wa kwanza walivunja mkate na kunywa kikombe kila siku ya Bwana (Matendo 20:7). Walitoa zawadi zao siku yenyewe vilevile, ndiyo siku ya kwanza ya juma (l Wakorinto 16:2).

(3) **Maombi**. Kuna ahadi tamu sana kwa watu wawili au watatu wanaofungana pamoja katika maombi kwa kitu fulani (Matayo 18:19).

(4) Tunaona kusanyiko la watumishi wa kanisa ndani ya Matendo 6.

**Sharti kanisa la pahali fulani lisimame kwa utaratibu gani?**

Mungu ni Mungu wa utaratibu. Dunia hii na hata ulimwengu mzima zinatembea kwa utaratibu. “Mungu si Mungu wa machafuko” (1 Wakorinto 14:33).

Sharti tuwe na utaratibu ndani ya kanisa vilevile, utaratibu wa Mungu. Sharti mambo yote yatengenezwe na kufanywa kwa utaratibu wake. Tunaona utaratibu huu ndani ya Agano Jipya.

Kulikuwa na watu wa namna tatu ndani ya kanisa kwa Filipi: watakatifu, waangalizi na watumishi (Wafilipi 1:1). Watakatifu wote walikuwa makuhani vilevile.

**Waangalizi** walikuwa wanani? Leo tunaona mwangalizi mmoja (anaitwa askofu vilevile) akitawala juu ya makanisa machache. Lakini kwa Filipi kulikuwa na waangalizi kupita mmoja juu ya kanisa lile moja. Waliitwa wazee vilevile (Tito 1:5,7). Katika 1 Timoteo 3:1-7 na Tito 1:7-9 tunaona mambo gani yaliyo sharti kuonekana ndani ya maisha ya mwangalizi. Kazi yake kubwa ni kulinda kondoo za kundi la Mungu, ndio Wakristo ndani ya kanisa. Haifai ajitafutie mali kwa kazi hii kwani Bwana Yesu Kristo, Mchungaji Mkubwa, atampa zawabu yake wakati atakapokuja tena (1 Petro 5:4). Sharti Wakristo wakumbuke ya kwamba Bwana ameweka wazee hawa juu yao, na kuwatii (Waebrania 13:7,17).

**Watumishi** wanafanya kazi namna mbalimbali ndani ya kanisa. Wanachunga mali Wakristo wanazotoa kwa Mungu, au kuongoza chuo cha watoto siku ya Bwana, kuonyeshea wageni pahali pa kuketi nyumbani mwa Mungu, vivi hivi. Ni lazima kwa karibu mambo yote yaliyo sharti kwa mwangalizi kuonekana ndani ya maisha ya mtumishi vilevile. Ona 1 Timoteo 3:8-13. Katika Matendo 6 watu wa kanisa walichagua watumishi kuangalia maneno ya mali, lakini waangalizi wanachaguliwa na Bwana Yeye Mwenyewe.

Kristo anatoa zawadi kwa kanisa vilevile: wachungaji, walimu, wahubiri wa Habari Njema (Waefeso 4:11). Kusudi la kazi yao ni kukamilisha watakatifu kwa kazi ya utumishi, hata mwili wa Kristo ujengwe (Waefeso 4:12).

Zawadi hizi ni kwa mwili mzima wa Kristo. Lakini hatusomi hata neno moja ndani ya Agano Jipya juu ya kuunganisha makanisa fulani pamoja ili mtu mmoja au watu fulani wayaongoze. Neno hili "kanisa" linatumiwa ndani ya Biblia kwa mwili mzima wa Kristo tu, *au* kwa kanisa la mji au kijiji kimoja. Kila kanisa kwa pahali fulani lilihukumiwa na Kristo tu. Makanisa walikuwa na ushirika na upatano katikati yao, lakini hakuna kanisa lililokuwa na amri juu ya kanisa lo lote lingine na kuagiza Wakristo wa kanisa lile lingine nini iliwapasa kufanya.

# NINI ITATOKEA NYUMA?

Tumeona ya kwamba wokovu ndio habari kubwa sana. Tumeona ya kwamba tumepata wokovu hata sasa. Lakini hata kama tulipokea wokovu siku tulipoamini Kristo, kazi ya kutuokoa inaendelea hata leo. Tungali na tabia ya zambi. Hata Mkristo akitembea karibu sana na Bwana, anaweza kujaribiwa na zambi. Tabia hii ya zambi ita-ondoshwa kwake wakati Bwana Yesu Kristo atakapokuja.

Agano la Kale linafundisha ya kwamba Kristo atakuja. Mashairi mengine yanatupasha juu ya mateso atakayopata, kama Zaburi 22 na 69. Mengine yanatabiri habari za utukufu wake, kama Zaburi 2 na 72. Ilishinda manabii kufahamu namna gani mambo haya mawili yaliweza kuwa kweli (1 Petro 1:10-11). Sisi tunafahamu. Kristo alikuja kweli na aliteswa. Siku nyingine atakuja tena na utukufu.

Mashairi mengi katika Agano la Kale yanaleta habari juu ya kurudi kwa Kristo. Yesu Yeye Mwenyewe alisema, *"Kama nina-kwenda . . . nitakuja tena"* (Yoane 14:3).

Wakati tunaposoma na kuwaza sana juu ya mashairi yanayo-pasha habari za kuja kwa Kristo, tunaona tofauti nyingine. Nabii mmoja, akitabiri juu ya kuja kwa kwanza kwa Kristo, alisema atafi-ka kwa Betelehemu (Mika 5:2). Mwingine alisema atakuja ku Yerusalema akitembea juu ya punda (Zekaria 9:9). Unabii gani ulikuwa kweli? Manabii hawa wawili wote walitabiri habari za kweli. Bwana Yesu Kristo alifika duniani kwanza kwa Betelehemu kama mtoto mdogo (Matayo 2:1). Miaka 30 nyuma alijionyesha wazi kwa watu wa Israeli kama Mfalme wakati wa kuingia kwake katika Yerusalema (Matayo 21:1-11). Saa yenyewe unabii wa Zeka-ria ulitimizwa.

Vivyo hivyo, wakati tunaposoma juu ya kuja tena mara ya pili kwa Kristo, tunaona ya kwamba mashairi mengine yanapasha juu ya kuja kwake *kwa* watakatifu wake (Yoane 14:3), na mengine juu ya kuja Kwake *pamoja* na watakatifu wake (1 Watesalonika 3:13). Namna gani ataweza kuja *kwa* watakatifu wake na *pamoja* nao? Ndiyo, neno hili haliwezekani. Basi tumeona sawasawa hesabu

fulani ya miaka ilipita nyuma ya kuja kwake kama mtoto mdogo kwa Betelehemu na mbele ya kuingia kwake katika Yerusalema kama Mfalme. Au kusema kuja kwake kwa kwanza kulikuwa na sehemu mbili. Vivyo hivyo hesabu fulani ya miaka itapita nyuma ya kuja kwa Kristo KWA watakatifu wake mbele ya kuja kwake PAMOJA nao.

## KUPELEKWA KWA WAKRISTO MBINGUNI

Wakati Kristo atakapokuja KWA watakatifu wake, kuwapeleka mbinguni, watanyanyuliwa katika mawingu.

> *"Sisi sote . . . tutanyanyuliwa . . . katika mawingu, kukutana na Bwana katika hewa"* (1 Watesalonika 4:17).

Habari hizi ni mbali na kuja kwa Kristo katika utukufu. Ndani ya Agano la Kale tunasoma mara nyingi juu ya kuja kwake kama Mfalme, lakini Paulo anaita habari za kupelekwa kwa Wakristo mbinguni "siri" (1 Wakorinto 15:51). Siri ni neno ambalo watu hawalijui. Bwana Yeye Mwenyewe alijulisha Paulo siri hii ("kwa neno la Bwana," 1 Watesalonika 4:15). Hivi tunaweza kujua ya kwamba hakuna mafundisho juu ya neno hili ndani ya Agano la Kale.

Tunapata mafundisho juu ya sehemu hii ya kwanza ya kuja kwa pili kwa Kristo katika 1 Wakorinto 15:51-56 na 1 Watesalonika 4:13-18. Tunaona ya kwamba:

Bwana atashuka toka mbinguni na sauti kubwa.

Waamini waliokufa mbele watafufuliwa kwanza toka wafu.

Waamini walio kwanza hai watageuzwa na kupewa miili mipya.

Wao wote watanyanyuliwa katika mawingu.

Mambo haya yatatokea mbio kabisa, kwa dakika moja, kwa kufunga na kufungua jicho.

Halafu watakuwa pamoja na Bwana kwa milele.

Hii ndiyo taraja tamu sana, taraja nzuri kabisa ya kila mwamini, "tumaini la baraka" (Tito 2:13). Lakini tukumbuke vilevile ya kwamba "kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe mbele ya Mungu" (Waroma l4:12).

> *"Imetupasa sisi sote kuonekana mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo"* (2 Wakorinto 5:10).

Usifikili waamini watahukumiwa kwa zambi zao kwa kiti cha hukumu cha Kristo. Sivyo. Biblia inatufundisha wazi ya kwamba

*"hakuna hukumu YA AZABU juu yao walio katika Kristo Yesu"* (Waroma 8:1).

Halafu nini itatokea kwa kiti cha hukumu cha Kristo? Kristo atatupa sisi zawabu kwa kazi yo yote ambayo tuliifanya kwa utukufu wake. Wengine watahuzunishwa sana wakati watakapoona kazi zao zikiteketea ku moto. Kwa sababu gani zitateketea kwa moto? Kwa sababu wale ambao walizitenda hawakuzitenda kwa kupendeza na kutukuza Mungu, lakini kwa kujipatia wenyewe heshima na faida. Hata hivi wataokolewa wao wenyewe (1 Wakorinto 3:13-15). Wale watakaopokea taji wataziweka kwa miguu ya Mwokozi, kwa kuongeza kidogo kipimo cha heshima na utukufu atakazopata siku ile (Ufunuo 4:10).

Ndoa ya Mwana-Kondoo itafuata kiti cha hukumu cha Kristo (Ufunuo 19:1-8). Utakuwa wakati wa furaha kubwa, kwa watakatifu na kwa Mwokozi vilevile, mwanzo wa wakati wa milele wa furaha ya kuzidi mbinguni.

## MATESO MAKUBWA

Tangu zambi ilipoingia duniani, taabu na huzuni zinazidi. Kuna tufani na matetemeko ya inchi. Njaa, magonjwa na vita zimeua milioni za watu.

Lakini Biblia inafundisha juu ya wakati wa mateso makubwa zaidi (Ufunuo 7:14). Tunasoma juu yake katika Matayo 24:4-29. Shairi 21 linasema yatakuwa mateso makubwa kupita mateso yote mengine tangu kuumbwa kwa mtu. Katika Ufunuo sura 6-18 tunasoma habari nyingine kwa mifano. Utakuwa wakati wa taabu kupita yote ambayo watu waliijua mbele. Labda Wayuda waaminifu watakaokataa kuinama mbele ya sanamu watateswa kwanza, kisha Wayuda wote. Mungu anawaacha kuteswa kwa sababu taifa lao lilisulibisha Mwana wake. Halafu Mataifa watachukia na kutesa Wayuda kupita kipimo na gazabu ya Mungu itapata mataifa yote mengine vilevile.

Mateso haya yatasukuma watu kutubu zambi zao? Hapana, hata kidogo! Kwanza watajazwa na woga (Ufunuo 6:15-17); nyuma watatukana jina la Mungu.

*"Hawakutubia kazi ya mikono yao . . . wakatukana jina la Mungu"* (Ufunuo 9:20-21; 16:9,11).

Tangu zamani Mungu ameonyeshea watu neema, lakini watu wanazidi kuendelea ndani ya zambi zao. Labda watu wengine wanafikili: "Kama Mungu akiazibu mtu kwa zambi zake angali yeye ni hapa duniani, mtu huyu atajua ya kuwa Mungu amekasiri-

ka, na atatubu na kurudi karibu na Mungu." Lakini sivyo. Hata wakati Mungu anapoonyesha gazabu yake wazi kabisa, watu hawatubu. Mateso Makubwa yanaonyesha hivi.

Maneno haya yatatokea wakati gani? Mateso Makubwa yatafuata kupelekwa kwa Kanisa mbinguni (Ufunuo 3:10) na yatatangulia kurudi kwa Kristo katika utukufu. Yataendelea kwa miaka mingapi? Hayataendelea kwa muda mrefu (Matayo 24:22). Nabii Danieli alitabiri kutakuwa na miaka saba ya ukiwa (Danieli 9:27). Wakristo wa kweli watakuwa wapi kwa wakati ule? Pamoja na Yesu mbinguni.

## KUJA KWA PILI KWA KRISTO

Mateso Makubwa yatakwisha gafula wakati Kristo atakapotokea duniani.

> *"Mara moja nyuma ya mateso ya siku zile . . . wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa"* (Matayo 24:29-30).

Halafu nini itatokea? Kristo ataonekana kwanza kwa watu wa Mungu wa zamani, ndio Waisraeli. Watakuwa na huzuni nyingi wakati watakapokumbuka namna taifa lao lilivyokataa Masiya yao wenyewe (Zekaria 12:10).

Kisha mataifa walio hai watahukumiwa (Matayo 25:31-46). Watu wa mataifa walioonyesha imani yao kwa Mungu kwa njia ya kusaidia watu wake Wayuda watapewa ruhusa kuingia ufalme wa Kristo duniani. Wengine wataazibiwa kwa milele. Wakati wale waovu watakapokwisha kuondoshwa, Kristo atasimamisha ufalme wake duniani.

Tangu zamani tumaini la kurudi kwa Kristo ni faraja kubwa kwa watu wa Mungu. Lakini kuna watu wengine wanaocheka maneno haya. Kwa siku za mwisho watabisha kweli hii ya kurudi kwa Kristo na roho ya uchungu (2 Petro 3:3-4).

Watu wanaamini vilevile mambo mengine yasiyo kweli:

1. Wengine wanafikili Kristo "anakuja" wakati anapoingia rohoni mwa mtu anayeamini. Au, wakati mtoto wa Mungu anapokufa, Kristo "anakuja" kwa roho ya mtu huyu. Ndiyo, kwa njia nyingine maneno haya ni kweli, lakini Biblia inafundisha wazi ya kwamba Kristo atarudi Yeye Mwenyewe, katika mwili.

> *"Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni"* (Matendo 1:11).

2. Watu wengine wanafundisha Kanisa litakuwa duniani kwa wakati wa Mateso Makubwa ili lisafishwe toka zambi zake. Lakini tukumbuke ya kwamba mwamini haazibiwi kwa sababu ya zambi zake (Bwana Yesu Kristo alibeba azabu hii juu ya msalaba), lakini Mungu anamfundisha asifanye zambi tena. Mateso Makubwa ni kuazibu wasioamini kwa zambi zao.

3. Wengine wanasema sehemu ya Kanisa itakuwa duniani kwa wakati wa Mateso Makubwa, ndio waamini wale wasiotii Bwana hapa duniani. Kama ikiwa hivi, viungo vingine vya mwili wa Kristo watakuwa wakifurahi mbinguni wakati vingine watakapopata mateso makubwa hapa duniani. Hatuoni mafundisho haya ndani ya Biblia. Kristo hawezi kupumzika kufika wakati watu wake wote, **mwili wake mzima**, watakapokuwa pamoja naye pahali alipo.

4. Halafu kuna watu wanaosema Bwana atakuja mwaka fulani na siku fulani. Lakini hatuwezi kujua siku gani Bwana atakapotokea. Wakati Bwana Yesu alipokuwa hapa duniani alisema Yeye Mwenyewe hajui siku gani atakapokuja (Marko 13:32).

Kabisa kabisa ni vizuri kwa sisi kuwa wajinga katika kujua wakati gani Kristo atakaporudi. Tukifikili kila siku, “Labda Bwana atakuja leo,” mawazo haya yatatusaidia kujichunga na roho safi, tayari kwa kurudi kwake, na yatatuzuiza tusifanye kitu tutakachopata haya juu yake kama Bwana akitukuta tukifanya kitu chenyewe wakati atakapotokea.

*“Kila mwenye tumaini hili katika yeye*
*anajitakasa mwenyewe”*
(1 Yoane 3:3).

# WAKATI WA KUJA

Manabii wa zamani wakiongozwa na Mungu walitabiri juu ya wakati wa furaha utakaokuja. Wakati ule watu wote watabarikiwa kwa njia ya Mungu Mwana. Muda huu wa baraka unaitwa vilevile Ufalme wa Kristo.

## MIAKA ELFU MOJA

Katika Ufunuo 20:4 tunasoma ya kwamba Kristo atatawala kwa miaka elfu moja. Utawala huu utakuwa namna gani?

(1) Kwa sababu ya zambi ya Adamu udongo ulilaaniwa (Mwanzo 3:17-18). Unaotesha miiba sasa. Lakini kwa wakati wa kuja maua yataota tena ndani ya jangwa (Isaya 35:1). Nyama za mwitu hawatakuwa wakali tena (Isaya 65:25), na nyama zote hawatapata taabu tena (Waroma 8:19-22).

(2) Mataifa ya dunia watakuwa na mali nyingi kupita mbele. Vita haitakuwa tena (Isaya 9:7). Fikili juu ya mali nyingi inayohitajiwa kwa kulipa wapolisi na askari, hata wakati wa salama! Wakati Kristo atakapotawala, mambo haya hayatahitajiwa tena.

Watu wachache tu watakuwa wagonjwa au watakufa. Watu wataishi kwa miaka mingi na kuwa wazee kabisa (Isaya 65:20). Hesabu ya watu watakaokuwa duniani wakati ule itapita mbali hesabu ya watu wakati wa sasa. Lakini Kristo Mfalme ataangalia ili wao wote wawe na vitu vyote wanavyohitaji.

Wote watakaoingia Ufalme huu watakuwa wana wa Mungu. Lakini itapasa watoto wao kuzaliwa tena. Labda zaidi yao wataamini. Hata wale wasioamini watalazimishwa kutenda kwa haki, au wataazibiwa (Isaya 11:4-5). Shetani atafungwa kwa miaka elfu moja (Ufunuo 20:2).

(3) Taifa la Israeli litakuwa kiongozi katikati ya mataifa ya dunia (Isaya 60:12). Litapewa heshima hii na Mfalme wa Israeli, Bwana Yesu Kristo. Mitume watasaidia Kristo ndani ya kazi ya kutawala Israeli (Matayo 19:28). Watu wengine wengi watashiriki katika kazi ya kutawala Israeli, lakini kazi yao haitakuwa kazi ya heshima sana kama ile ya mitume (Luka 19:17,19). Watawala hawa watakuwa Wayuda waliokuwa waaminifu kwa Kristo wakati alipokataliwa. Wakristo ni viungo vya mwili wa Kristo. Kama bibi arusi yake,

watakwenda pamoja naye pahali po pote Yeye atakapokwenda. Anataka sana waweze kuwa pahali alipo (Yoane 14:3).

Bila shaka wakati Kristo atakapokuja kutawala, mambo yote yatakuwa mazuri sana hapa duniani. Yataonekana kuwa makamilifu kabisa. Lakini hata hivi kutakuwa na watu wengi wakati ule wasiopenda Bwana kweli. Watatii tu kwa sababu ya lazima. Lakini wakati watakapopata njia, wataasi.

Kwa mwisho wa utawala wa Kristo wa miaka elfu moja Shetani atafunguliwa kwa muda mufupi. Atakusanya watu hawa wasioamini Kristo kweli kweli. Watajaribu tena (hii ni mara ya mwisho) kushindana na watakatifu, lakini watashindwa. Moto toka mbingu utawaharibu. Shetani na wasaidizi wake watatupwa ndani ya ziwa la moto (Ufunuo 20:7-10).

Ufufuko wa pili utafuata. Tumeona mbele sawasawa wale waliokuwa waamini wa kweli wakati wa kufa kwao watafufuka wakati Bwana Yesu atakaporudi, mbele ya kusimamishwa kwa Ufalme wa Kristo. Kwa mwisho wa Ufalme huu waovu watafufuliwa (Yoane 5:28-29). Usifikili waamini tu watafufuliwa toka wafu. Kwa sababu Kristo alifufuliwa toka wafu, watu wote watafufuka vilevile (1 Wakorinto 15:22).

Kwa Kiti Kikubwa Cheupe vitabu vitafunguliwa. Kila mtu atahukumiwa sawasawa na maneno haya yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yake. Mwana wa Mungu ataketi juu ya kiti hiki cha kifalme (Yoane 5:22). Anajua mambo yote na atahukumu kwa haki. Kwa sababu aliishi hapa duniani Yeye Mwenyewe, anaweza kufahamu shida na uzaifu wa watu. Lakini hakuna wokovu kwa wale waliokataa kupokea Kristo kuwa Mwokozi wao wakati walipoishi duniani. Majina yao hayatapatikana ndani ya kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo. Watapelekwa kwa ziwa la moto lililotayarishwa kwa Shetani na malaika zake.

*Hadeze* ni nini? Ni wapi? Bwana Yesu alisema maneno ya kuogopesha juu ya hali ya wapotevu: *"giza la inje . . . kulia na kusaga meno"* (Matayo 8:12; 22:13; 25:30).

Yuda anasema waovu watakuwa kama "nyota zinazopotea . . . weusi wa giza umewekwa akiba kwao hata milele" (Yuda 13). Hatujui pahali Hadeze ilipo. Tunajua tu ni mbali sana na Mungu.

Biblia haitupashi maneno mengi juu ya mbingu vilevile. Tunasoma tu ya kwamba mambo mengine hayatakuwa mbinguni: huzuni, kutoa machozi, kuumia, laana, mauti. Lakini nuru na uzima na mapendo na utukufu zitakuwa.

## WAKATI WA MILELE

Wakati huu wa sasa ni kama pwani nyembamba iliyo na bahari kubwa kwa kuume na kwa kushoto. Hatujui kama maneno yetu ya sasa yataendelea kwa miaka mingapi. Mbele ya kuumbwa kwa dunia, kulikuwa na muda usio na kipimo, muda wa milele. Na wakati habari zetu za sasa zitakapokwisha, kutakuwa na muda mwingine usio na kipimo, muda wa milele kwa wakati wa kuja.

*"Tangu milele na hata milele wewe ni Mungu*" (Zaburi 90:2).

Hatujui kama milele ni muda wa miaka mingapi. Tunajua tu ni wakati usio na mwisho.

Dunia hii imechafuwa na zambi. Ni kusudi la Mungu kuiharibu kwa moto na kuumba dunia mpya (2 Petro 3:10-13). Ataumba mbingu mpya vilevile. Isaya alisema ya kuwa dunia ya kwanza haitakumbukwa tena (Isaya 65:17). Yoane aliona ndani ya maono mbingu mpya na dunia mpya (Ufunuo 21:1). Ndani ya dunia mpya haki itapanga (2 Petro 3:13).

Ndani ya elfu za miaka iliyopita Mungu amejifunua kwa njia mbalimbali. Kulikuwa na wakati wa sheria, wakati wa neema, wakati wa ufalme. Kwa miaka ya kuja tutaendelea kujifunza zaidi juu ya Mungu (Waefeso 2:7). Tutapata majibu kwa maulizo yetu yote, mambo tusiyoweza kufahamu hapa duniani. Ndiyo, Mungu tu anaweza kujua mambo yote. Lakini wakati ule hata watu watajua kupita sasa.

Watu wengine wangependa kufikili ya kwamba waovu hawatakuwa tena, au kusema hawatakuwa na mwili, nafsi na roho tena kwa kusikia kuumia na huzuni. Lakini neno linalotumiwa ndani ya Biblia kwa azabu YA MILELE ni neno lile lile linalotumiwa kwa Mungu WA MILELE (Ufunuo 14:11; 15:7). Ni huzuni kubwa, lakini ni kweli ya kama watu waliokataa Kristo watatengwa na Mungu na kuteswa kwa milele. Taabu yao haitakwisha kamwe.

Neno hili "milele" linatumiwa kwa baraka ya waamini vilevile (Ufunuo 22:5). Tutakuwa pamoja na Kristo (Yoane 17:24). Tutakuwa wariti pamoja naye (Waroma 8:17). Tutakuwa sawasawa naye (1 Yoane 3:2). Tutashiriki mambo ya kupendeza kwa mkono wake wa kuume kwa milele na milele (Zaburi 16:11).

***Kweli BWANA anastahili***
***kupokea sifa zote!***